SUPA JACKPOT
TZS. 1,067,615,605
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 8

**WAZIRI** Mkenda ashtukia jambo digrii ya udokta wahitimu wa nje


KUKOMA KWA MGOGORO ARDHI MIAKA 15...
Uamuzi wa Rais ulivyowaondolea mhemko, ukawasogezea tabasamu wakazi Mbarali
Ukurasa 12
PENYE NYUFA KISIASA, KIUCHUMI PANABOMOA UKUTA.. Rais Samia kafungulia mikutano ya kisiasa, zamu ya vyama sasa kulinda mitaji uchumi
Ukurasa 13
Hivi Watanzania tunajisikiaje kubagaza Kiswahili?
BUFE
IJUMAA JANUARI 20, 2023
Nipashe
Ukurasa 14
Japan; kinara wa madeni duniani
NA Juma Mpagama, MBARALI
NI hatua ya kupumua, kunakosindikizwa na tabasamu kuanzia kwa wakazi hadi kwa watendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbarali, mkoani Mbeya, jalada na mgogoro wa ardhi kumalizwa.
Ni uamuzi mgumu uliochukuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutatua mgogoro wa ardhi mkoani hapo, ulioudumu kwa miaka 15, ukiwahusisha wananchi wa Bonde la Usangu na kwenye Hifadhi ya Taifa Ruaha, hata ikawa inaleta kadhia kubwa ya kijamii.

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Januari 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581196

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Mtoto akutwa akinyonya titi la mama aliyeuawa

**MAITI** ilikuwa imefungwa mikono... *Endelea ukurasa 2*



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, George Katabazi



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Spika wa Bunge la India, OM Birla, kwa niaba ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Spika wa India asifu utendaji wa Rais Samia

UKURASA 3

UKURASA WA 3

## MWANAFUNZI ACHANGIA MILIONI 100/- KUSAIDIA WATOTO WENYE USONJI

MWANAFUNZI wa kidato cha nne Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Madeleine Kimario, amechangisha Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia mazoezi tiba kwa watoto wenye tatizo...

## Polisi watanda kwenye kanisa alilosimamishwa Mch. Kimaro

UKURASA 2

MICHEZO ROBERTINO AWATULIZA MASHABIKI MSIMBAZI UK. 24

KATUNI UK. 6



Mkurugenzi wa Kampuni ya Vanilla International, Simon Mkondya, akionyesha moja ya mmea wa vanilla, wakati akitoa elimu namna ya kulima zao hilo, kwa baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga jana, ili kuwaongezea kipato cha kaya, kwa madai kuwa kilo moja ya vanilla inanunuliwa kwa Sh. milioni moja hapa nchini. Habari Uk. 10. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mtoto akutwa akinyonya titi la mama aliyeuawa

**Na Beatrice Shayo**

NI tukio la kusikitisha, mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja amekutwa usiku akiendelea kunyonya ziwa la mama yake ambaye anadaiwa kuuawa na mumewe, Jeshi la Polisi mkoani Manyara limethibitisha.

Katika uhalifu huo dhidi ya mama huyo, Sabina Barma (28) ambaye maiti yake ilikutwa imefungwa mikono, inadaiwa kifo chake kimetokana na kudhuriwa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali shingoni akiwa nyumbani kwake.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Gisigisi, Kijiji cha Saydoda, Kata ya Ufana wilayani Babati, John Manonga, alisema walimkuta mtoto akinyonya ziwa la mama yake, bila ya kujua kuwa ameshafariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, George Katabazi, alithibitisha mwanamke huyo aliuawa juzi majira ya saa tatu usiku.

Alidai chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi na kwamba mumewe anayesadikiwa kufanya uhalifu huo, alikimbia na kwenda kusikojulikana baada ya kutekeleza mauaji hayo.

"Mwili wa marehemu umekutwa na majeraha kwenye shingo, alichomwa na kitu chenye ncha kali. Jeshi la Polisi tunaendelea kumsaka mume wake ambaye alikimbia baada ya tukio hilo na kama kuna yeyote anayejua alipo, tunaomba mtujulishe," alisema.

Kamanda Katabazi alitoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na kusababisha watu kupoteza uhai wao.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Kitongoji cha Gisigisi yaliyotokea mauaji hayo, mama huyo ameacha watoto watano.

Mwenyekiti huyo aliviomba vyombo vya dola kuhakikisha vinamkamata mtuhumiwa huyo ili liwe fundisho kwa wengine ambao wana nia ya kutenda vitendo vya aina hiyo.

Mmoja wa mashuhuda, aliyeomba hifadhi ya jina lake, alidai kuwa mama huyo alikuwa amefungwa mikono na kuchomwa shingoni kwa kitu chenye ncha kali na maeneo mbalimbali ya mwili wake.

"Tulimkuta marehemu alikuwa na kamba mkononi, inaonyesha huyo mume wake alimtesa sana... shingoni amechomwa na kitu chenye ncha kali," alidai.

Kutokana na mauaji hayo, kumeibuka mgogoro, wazazi wa marehemu wakiamua kuitenga familia ya mumewe, wakichukua mwili wa ndugu yao kwa ajili ya maziko nyumbani kwao na watoto kulelewa na familia ya marehemu.

Haki ya kuishi imetajwa kikatiba. Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria".


**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA/NOTISI**

**TANFIN CONSULTANT E.A LTD** Kwaniaba ya **ARUSHA WOMEN IN BUSINESS SACCOS LTD** Tunatoa notisi na Tangazo la mnada kwa Wanadaiwa na wadhamini wao wanaosomeka hapa chini wawe wamelipa deni lao wanalodaiwa na **SACCOS** hiyo kinyume na hapo tutauza dhamana na mali zao kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada utafanyika sehemu dhamana/mali husika ilipo na tarehe kama inavyotangazwa hapo chini

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | GETRUDE MATHIAS TEMBA | NYUMBA ILIOPO MTAA WA KAMBI YA FISI KATA YA NGARENARO JIJINI ARUSHA | 10/02/2023 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | GLORY FEDINAND MASSAWE | KIWANJA KILICHOPO KITONGOJI CHA CHEM CHEM KATA YA IMBASENY MAJI YA CHAI ARUMERU MKOANI ARUSHA | 10/02/2023 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnada utafanyika sehemu dhamana ilipo na zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) italipwa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 kiasi kilicholipwa awali cha 25% utarudiwa wa tena.
3. Gharama za kubadilisha umiliki (TRANSFER OF OWNERSHIP) pamoja na gharama nyingine zinazohusiana na umiliki wa mali hizi ni juu ya mnunuzi.

**Mobile: 0785 944 141, 0764 525 592**

17236702


# Polisi watanda kanisa alilosimamishwa Kimaro

**Na Mary Geofrey**

SAKATA la kusimamishwa kazi kwa Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, limeendelea kuwa gumzo huku askari wakionekana kufanya doria kanisani huko.

Juzi usiku kwenye ibada ya 'masifu ya jioni', askari polisi walionekana wakizunguka nje ya kanisa hilo wakati ibada ikiendelea ndani ya kanisa.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alipozungumza na Nipashe kuhusu suala hilo, alisema doria za askari polisi ni za kawaida kwenye maeneo mbalimbali ya jiji hilo la kibiashara.

"Nikuulize kabla ya hilo sakata, hukuwahi kuona askari wakizunguka kanisani hapo? Hizi ni doria za kawaida na haihusiani na jambo hilo," alisema Kamanda Muliro.

Ikiwa ni siku ya nne tangu kuibuka kwa mvutano huo, juzi Nipashe iliwashuhudia waumini wakiendelea kufanya ibada nje ya kanisa wakati ibada ya masifu ya jioni hufanyika ndani ya kanisa.

Wakiwa nje ya kanisa hilo, waumini hao walimba nyimbo za kumsifu Mungu na kumwombea Mch. Kimaro.

Katika kuhakikisha usalama unaimarishwa kwenye kanisani hilo, kila aliyekuwa anaingia, getini aliulizwa majina na namba za mtaa anaotoka.

Mchungaji Kimaro alisimamishwa kuendelea na huduma ya kichungaji katika usharika huo kwa siku 60 pasi na kuwekwa wazi sababu za adhabu hiyo.

Tangu Jumanne uongozi wa Dayosisi hiyo umekuwa ukitafutwa na waandishi wa habari kuzungumzia sakata hilo bila ya mafanikio.

Katibu Katibu Muktasi aliyekutwa katika ofisi hizo jana, alimweleza mwandishi wa Nipashe kuwa viongozi wote, akiwamo Askofu wa Dayosisi hiyo, Alex Malasusa, Msaaidizi wa Askofu, Lwiza na Katibu Mkuu, Goodluck Nkini, wapo nje ya ofisi kwa ajili ya vikao.

"Viongozi wote hao hawapo, wameenda kwenye vikao nje ya ofisi, kwa hiyo huwezi kuwapata kwa sasa, ahsante na karibu tena," alisema katibu huyo.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Frederick Shoo, juzi alikaririwa na vyombo vya habari akieleza kupata habari za kusimamishwa kwa mchungaji huyo kupitia mitandao na kuwataka waumini wa usharika wa Kijitonyama na wakristo kuwa watulivu.

"Tutambue kuwa dayosisi ina vyombo vyake vya uamuzi na bila shaka jambo lenyewe linaendelea kufanyiwa kazi na dayosisi husika, baadaye sisi ambao tumepokea taarifa kama hizi tunaendelea kufuatilia na kupata taarifa zaidi kuhusu jambo hili ambalo linaonyesha limeleta usumbufu na mwitikio tofauti kutoka kwa watu wengi.

"Kubwa sana ambalo ningeomba wakristo hawa na waumini wa usharika wake, waweze kuwa watulivu wakati jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi," alisema Askofu Shoo.

Muumini wa kanisa hilo, Judith Jude alisema jana kuwa: "Hatuwezi kutoa sadaka zetu kanisani wakati mchungaji wetu kafukuzwa kama mhalifu, tulipaswa tuambiwe ili aagwe, aende anakotakiwa kupelekwa na siyo kuondolewa wakati akiwa anaendelea na semina."

Wakati akitangaza uamuzi huo, Mch, Kimaro alisema: "Nimepewa barua ya likizo ya siku 60, kwa hiyo ninatumia fursa hii kuwaaga, kesho asubuhi atahubiri Mch. Anna na ndiye atakuwa mchungaji wenu, kwa mujibu wa barua nitarudi Machi 17 na sitakuja hapa, barua inanielekeza kuripoti makao makuu ya dayosisi."

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe (kushoto), akipokea msaada wa Sh. milioni 100 kutoka kwa Mwanafunzi wa Kidato cha Nne wa Shule ya Sekondari ya Kimataifa IST, Madeleine Kimaro (wa pili kushoto), jijini Dar es Salaam jana, alizochangisha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kutoa huduma za mazoezi tiba kwa wanafunzi wasiopungua 15 katika Kituo cha Msimbazi Mseto Ilala kitengo cha Usonji. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Spika wa India afurahia utendaji kazi wa Samia

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge la India, Om Birla, amesema nchi yake inaridhishwa na utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ndiyo maana miradi mipya ya uwekezaji 630 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 3.68 inatekelezwa na kampuni za India nchini Tanzania.

Spika Birla pamoja na ujumbe wake kwa ziara ya kikazi ya siku tatu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati ujumbe wa Bunge la India (Lock Sabha) ulipokutana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa niaba ya Rais Samia.

Alisema, pamoja na mambo mengine atatembelea vituo mbalimbali vya utalii, ikiwamo mbuga za wanyama na fukwe za bahari.

Alisema kwa sasa Tanzania kuna mazingira wezeshi kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi, huku uchumi wake ukiendelea kustawi na kuwapa imani wanaotamani kuwekeza fedha zao kwenye sekta mbalimbali.

"Kwa niaba ya serikali na Bunge la India, tunawasilisha pongezi zetu kwa Rais Samia na uongozi wake wa mfano, sasa tunaona uchumi wa Tanzania unakuwa kwa kasi na tunaona miradi mikubwa ikitekelezwa, tafadhali fikisha pongezi zetu kwake."

Birla alisema Bunge la India litakuwa msemaji mzuri wa ushirikiano na maendeleo baina ya nchi hizo mbili ili ziendelee kunufaika na ushirikiano wao.

Waziri Mkuu Majaliwa, alisema kuongezeka kwa kampuni za India zinazowekeza nchini kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kunatokana na jitihada mbalimbali za kuboresha mazingira ya uwekezaji zilizofanywa na serikali.

Aliwakaribisha wawekezaji wengine kutoka nchini India kuendelea kumiminika na kuwekeza nchini na kwamba serikali itawahikishia mazingira salama na wezeshi muda wote, kwa kuwa lengo ni kukuza uchumi, kuongeza ajira na ustawi wa wananchi wa nchi hizo.

Kwa mujibu wa Majaliwa, India na Tanzania zimekuwa na ushirikiano mkubwa wa kiuchumi na biashara huku India ikishika nafasi ya tatu kwa kuwa na ushirikiano wa biashara unaofikia bilioni 4.58 kwa mwaka 2021 - 2022.

Uwiano wa kibiashara baina ya nchi zetu uko sawa, hivyo sote tunanufaika,"alibainisha.

Aidha, alimhakikishia Spika huyo kuwa Tanzania itaendeleza ushirikiano wa muda mrefu uliopo katika mataifa hayo.

"Rais anamatumaini makubwa na ushirikiano uliopo baina ya nchi ya Tanzania na India na kwamba ushirikiano huo umekuwa na manufaa makubwa kati ya nchi zetu."

Alisema nchi hizo zina ushirikiano wa muda mrefu katika sekta mbalimbali zikiwamo za uchumi, nishati, maji, elimu, afya, biashara na teknolojia na kuleta manufaa makubwa.

"Mheshimiwa Rais amefurahia ujio wako nchini Tanzania, ni matarajio yake kuwa ujio huu utakuwa na manufaa baina ya nchi zetu."

"Mwezi Juni 2022 tumeshuhudia kampuni sita kutoka nchini India zikitia saini mikataba ya miradi ya maji kwa miji 28 yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 500 ambayo ikikamilika itawawezesha Watanzania zaidi ya milioni sita kupata maji ya uhakika."

"Nitoe wito kwa nchi ya India ambayo kwa sasa ni mwenyekiti wa nchi za G 20, kuwa mtetezi wa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania katika suala zima la mabadiliko ya hali ya hewa, usalama wa chakula, uwezeshaji wa wanawake na vijana pamoja na kupambana na athari za Uviko-19," alisema.

Kadhalika, Majaliwa alisema ujio wa Spika huyo na ujumbe alioongozana nao utaboresha uhusiano baina ya Bunge la Tanzania na India kwa wabunge na viongozi kubadilishana uzoefu.

"Nitoe wito kwa mabunge yetu haya kuweka utaratibu wa kutembeleana na kubadilishana uzoefu, ili kukuza ushirikiano."

Pia Majaliwa aliishukuru Serikali ya India kwa ushirikiano na namna inavyoendelea kutoa fursa za masomo kwa wataalamu wa Tanzania katika sekta mbalimbali na kuiomba nchi hiyo kuendelea kutoa ufadhili huo katika nyanja nyingine za teknolojia ya mawasiliano, afya, uhandisi, kilimo, maji, madini na gesi.

# Wanafunzi wagoma kuishi katika hosteli

**Na Julieth Mkireri,**
KISARAWE

TABIA ya baadhi ya wanafunzi kugomea kujiunga na hosteli ili kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni inaelezwa kuwa chanzo cha kushuka ufaulu wilayani Kisarawe.

Vilevile, imeelezwa kuwa tabia wazazi kuwataka watoto wao kufeli kwenye mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi ili wapate muda wa kuchezwa ngoma na baadaye kuolewa, ni sehemu ya tatizo.

Akizungumza katika kikao cha kutathmini ufaulu wa mitihani shule za msingi na sekondari, Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Kisarawe, Editha Fue, alisema licha ya serikali kujenga hosteli za kisasa bado kumekuwa na hali ya kusuasua kwa wanafunzi kuishi.

Alisema tabia hiyo inatajwa kukwamisha jitihada za serikali za kuwanusuru wanafunzi na tabia ya utoro pamoja na mimba za utotoni.

Aidha, alieleza sababu nyingine kuwa ni pamoja na ukosefu wa chakula shuleni, hali ambayo inachangia baadhi ya wanafunzi kushindwa kusoma wakiwa na njaa.

Ofisa Elimu Msingi, Hadija Mwinuka, alisema wazazi wanatakiwa kuelimishwa kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao ili waondokane na tabia ya kuwalazimisha kufeli ambazo zinadumaza elimu.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Nickson Saimon, alielekeza kwa wale wanaopata vibali vya kuandaa sherehe kuhakikisha hakuna mtoto anayeshiriki kwenye ngoma hizo mchana na muda wa mkesha kwa kuwa kufanya hivyo ni kukwamisha ukuaji wa mtoto kimaadili na kielimu.

Saimon alisema serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha wanashirikisha walimu na wazazi, ili kuongeza jitihada za ufuatiliaji wa mwenendo wa wanafunzi ambao utamjenga mwanafunzi kimaadili.

# Mwanafunzi achangia milioni 100/- kusaidia watoto wenye usonji

**Na Mary Geofrey**

MWANAFUNZI wa kidato cha nne Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST), Madeleine Kimario, amechangisha Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia mazoezi tiba kwa watoto wenye tatizo la usonji.

Madeleine alikabidhi hundi ya fedha hizo kwa Asasi ya Kijamii ya Lukiza Autism Foundation, itakayotekeleza mradi huo wa mwaka mmoja kwa wanafunzi 15 wenye usonji katika Kituo cha Msimbazi Mseto wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya makabidhiano hayo, Madeleine alisema amechagua kufanya mradi wa usonji kwa sababu nchini tatizo hilo limekuwa haliongelewi na kupewa kipaumbele.

"Watu wengi hawajui kama hawa watoto wanapata shida, hivyo nimeamua kukusanya fedha hizi kutoka kwa watu wengi na kuleta hapa kwa Lukiza Foundation ili waweza kuwasaidia watoto hawa kwa mwaka mmoja," alisema Medeleine.

Alifafanua kuwa alikusanya fedha hizo kwa kuandika barua kwa kumtumia mtu mmoja mmoja, ambao walijitoa kufanikisha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Lukiza Autism Foundation, Hilda Nkabe, alisema mradi huo utawasaidia watoto katika mazoezi tiba ya mawasiliano na mazoezi tiba kazi.

"Sh. milioni 100 iliyochangishwa na mwanafunzi Madeleine ni kutokana na mradi wake umeendana na mradi wetu kuhusu usonji na kusaidia jamii na kutuchagua sisi na kutusaidia kuutekeleza kwa mwaka mmoja," alisema Hilda.

Mradi huo utashirikisha wataalamu wa mazoezi ambao watakuwa wakifanya kazi muda wote, kuwapatia wanafunzi chakula cha mchana shuleni, kutoa usafiri wa kuwafuata na kuwarudisha nyumbani kwa muda wa mwaka mmoja."

Aidha, alisema gharama za mradi huo kwa mwaka huu wa kwanza ni Sh. milioni 150 na kuwataka wafadhili wengine kuendelea kuunga mkono juhudi za Lukiza Autism Foundation ili kukamilisha mradi huu.

"Lengo la Lukiza Autism Foundation ni kutoa huduma endelevu kwa wanafunzi wote 45 waliko kituoni hapo kwa sasa," alisema Hilda.

Naye Ofisa wa Elimu Maalum, jijini Dar es Salaam, Swalehe Msechu, alitoa wito kwa wazazi na wanafunzi wote kuwapeleka watoto shuleni ili kupata huduma hizo badala ya kuwaficha.



Mkurugenzi wa Biashara kwa Wateja Wakubwa wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Adolfina William (kulia), akitoa maelezo kwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, kuhusu ushiriki wa benki hiyo, katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) Slot 4 kati ya Tabora na Isaka, mjini Isaka, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushahidi ulivyomweka huru mshtakiwa dawa za kulevya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imemwachia huru mfanyabiashara Bernad Silayo, maarufu Ben Mbuzi, baada ya Jamhuri kushindwa kuthibitisha kuwa alikamatwa na dawa za kulevya.

Uamuzi wa Mahakama ulitolewa mbele ya Jaji Godfrey Isaya kwenye masijala ndogo ya Moshi baada ya kupitia ushahidi wa upande wa Jamhuri na utetezi wa mshtakiwa.

Jaji Isaya alisema mshtakiwa anatuhumiwa kuwa Januari Mosi mwaka 2022, eneo la Njiapanda ya Himo wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro, alikamatwa na dawa za kulevya aina ya mirungi kilo 130.15.

Aliposomewa mashtaka, mshtakiwa huyo alikana kuhusika, upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Tully Helela na Mabuba Malima, ambao waliita mashahidi watano na vielelezo vinane.

Vielelezo hivyo ni ripoti ya Mkemia Mkuu wa Serikali, dawa za kulevya zilizokuwa ndani ya viroba sita, hati ya ukamataji mali na gari lenye usajili namba T 585 BSU aina ya Noah. Mshtakiwa alitetewa na Wakili Willence Shayo, upande huo wa utetezi ukiwa na mashahidi wawili na alitoa vielelezo viwili ikiwamo kadi ya gari na mkataba wa makabidhiano ya gari hilo aina ya Noah.

Katika shauri hilo, upande wa Jamhuri walidai Januari Mosi, 2022, majira ya saa 11 jioni, shahidi wa pili ambaye Ofisa wa Polisi, Sajenti Benald na Sajenti Mgeni walikuwa kwenye gari la polisi maeneo ya Himo.

Ilidaiwa mahakamani kuwa wakiwa huko, lilipita gari T 585 BSU Noah ambalo halikusimama, waliamua kulifuatilia na walipolifikia Sajenti Mgeni alimwambia dereva wa gari hilo asimame, dereva alisimama akashuka na kukimbia.

Askari hao walikwenda kukagua gari, ndani ya gari walikuta viroba sita ndani yake vikiwa na majani yaliyosadikiwa kuwa ni dawa za kulevya.

Hati ya ukamataji mali ilijazwa na kutiwa saini na askari hao na ripoti ya mkemia ilidai kuwa majani hayo ni dawa za kulevya aina ya mirungi.

Katika utetezi wake, pamoja na mashahidi wake wawili, mshtakiwa huyo alidai kuwa siku ya tukio, majira ya saa mbili asubuhi hadi saa tano usiku akiwa na mashahidi wake hao, alikuwa eneo la Marangu wakiuza supu.

Mshtakiwa alidai Desemba 27, 2021, mshtakiwa alimkabidhi gari hilo Gabriel Mchame kwa ajili ya biashara na shughuli za kanisa na sherehe za mwisho wa mwaka kwa makubaliano ya kumpa Sh. 40,000 kila siku kuanzia tarehe hiyo hadi Januari 5, 2022. Alidai kuwa Januari 5 ilipofika Gabriel hàkurejesha gari hilo ambapo Januari 7, 2022 alipata taarifa kutoka kwa kaka yake, Selestine Sirayo kuwa gari lake lilikuwa kituo cha polisi.

Alidai kuwa Januari 10, mwaka huo, aliamua kulifuatilia gari hilo polisi na ndipo alikamatwa na kuhojiwa kuhusu gari lakini alikana kuhusika na viroba sita vya mirungi.

Hata hivyo, alikiri kuwa gari hilo ni lake na alimkabidhi Gabliel Mchame.

"Ni takwa la kisheria kuwa ni wajibu wa upande wa mashtaka kuthibitisha shtaka pasi na kuacha shaka, mahakama imezingatia ushahidi wa pande zote mbili, imeona ushahidi wa shahidi wa kwanza na wa tatu wa upande wa mashtaka unajichanganya.

"Ushahidi unaonesha upekuzi ulifanyika njiapanda ya Himo lakini hati ya ukamataji mali ilikwenda kujazwa Kituo cha Polisi Kati Moshi, kwanini vyote havikufanyika njiapanda ya Himo, eneo la tukio?" Alisema jaji wakati wa kusoma hukumu.

# Uber yarejea, yaweka mambo sawa na serikali

**Na Gwamaka Alipipi**

KAMPUNI inayotoa huduma za usafiri wa kukodi kwa njia ya mtandao ya Uber, imetangaza kurejesha huduma zake nchini baada ya kufikia makubaliano na serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA).

Hatua hiyo imefikiwa baada ya LATRA kurekebisha vifungu vya kanuni vilivyokuwa vikisababisha kampuni hiyo kushindwa kutoa huduma ya usafiri kwa mtandao nchini. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Msimamizi wa Uber Tanzania, Monica Mziray, alisema kurejea kwao kutoa huduma kunatokana na makubaliano ya kurekebisha baadhi ya kanuni zilizokuwa zinawaminya kama kampuni.

"Tunaipongeza sana serikali kwa kuona umuhimu wa kupitia upya kanuni zilizokuwa zinatubana sisi kama kampuni, kwa sasa tunawatangazia Watanzania kuwa huduma zetu zimerudi kama zamani na tupo tayari kuwahudumia Watanzania," alisema Monica.

Meneja wa Uber Ukanda wa Afrika Mashariki, Imran Manji, alisema kuwa baada ya kufikia makubaliano na LATRA, kampuni hiyo imeondoa kesi iliyoifungua awali dhidi ya mamlaka hiyo.

"Huduma zote zilizokuwa zinatolewa kabla ya kusitisha huduma zitaendelea kutolewa huku usalama wa abiria na mali zao ukiimarishwa zaidi," alisema Imran.

Aliongeza kuwa kampuni katika kipindi chote ambacho walisitisha huduma, walikuwa wakijadiliana na serikali na kwa sasa mambo yamekaa sawa baada ya makubaliano ya pande zote mbili.

Mmoja wa madereva wa teksi mtandao kupitia Uber, Elikunda Materu alisema wamefarijika kuona huduma zimerejea, akisema uamuzi huo utaleta tija kwao kuendelea kujipatia kipato kupitia teksi mtandao.

Kampuni ya Uber ilisitisha huduma zake nchini Aprili mwaka jana baada ya kutokea mvutano na LATRA.

# Kampuni yapewa miezi 42 ujenzi SGR Tabora-Isaka

**Na Frank Monyo,** SHINYANGA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limeipa miezi 42 kuanzia Januari mwaka huu Kampuni ya Ujenzi ya Yapi Merkezi ya Uturuki kukamilisha kazi ya ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa (SGR) cha Tabora-Isaka chenye urefu wa Km 165.

Uzinduzi wa kipande hicho ulifanyika juzi kwenye Kijiji cha Isaka mkoani Shinyanga kwa kuwekwa jiwe la msingi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Katika hotuba yake, Dk. Mpango alisema: "Mradi huu wa SGR ni muhimu katika mkakati wa maendeleo ya Tanzania. Zaidi ya fursa 20,000 za ajira zimetengenezwa na jumla ya Sh. trilioni 1.9 zimekwenda kwa makandarasi wadogo, ambao wamelipa kodi zinazokuza Pato la Taifa."

Dk. Mpango aliipongeza TRC kwa juhudi za kuongeza thamani ya fedha kwa makandarasi wakubwa na wadogo.

"Ninawasihi makandarasi kufanya kazi kwa uadilifu na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati," aliagiza.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof Makame Mbarawa, alipongeza TRC kwa ushirikiano na mwongozo inaouonyesha katika mradi wa SGR na kuuhakikishia umma kwamba Serikali ya Tanzania imedhamiria kuwekeza katika miundombinu ya usafiri ili kuimarisha mifumo ya usafiri inayokwenda kukuza uchumi wa taifa.

Alisema takribani asilimia 14 ya Pato la Taifa limeongezeka kutokana na shughuli za usafirishahi bidhaa, huduma na watu.

Naibu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi ya Yapi Merkezi, Hana Alkan, alisema wamepewa kazi hiyo kutokana na uadilifu wao na ubora wa kazi waliouonyesha kwenye vipande vya reli viwili vya kwanza.

"Leo (juzi) tuna furaha kuongeza mradi mmoja mwingine tuliofanikisha kuufanya barani Afrika. Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania umetuzawadia awamu ya tatu na ya nne ya reli hii muhimu kutokana na uadilifu wetu na ubora wa kazi tuliouonyesha," alisema Alkan.

Alisema kampuni yake inatarajia kujenga miundombinu muhimu wakati wa utekelezaji mradi ambayo ni kujenga vituo vitatu katikati ya miji ya Tabora na Isaka, kituo cha marekebisho, eneo la mizigo, jengo la utawala, taasisi ya reli, reli yenye urefu wa Kilomita 165 na mifumo ya alama za mawasiliano na umeme.

Alisema Yapi Merkezi imetekeleza kwa umahiri miradi yake ya nyuma iliyofanyika nchi mbalimbali duniani na awamu ya nne ya ujenzi wa kipande hicho ni matokeo ya ukamilishaji mzuri wa awamu mbili za kwanza za mradi wa SGR Tanzania Dar es Salaam - Mwanza.

Mkurugenzi wa TRC Masanja Kadogosa alisema: "SGR itapunguza muda uliokuwa ukipotea kusafirisha bidhaa, huduma na watu, jambo litakalopunguza gharama za usafirishaji bidhaa na huduma pia.

"Kwa mfano, itachukua takribani saa nane kusafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza."

# MATANGAZO

## POSITION ANNOUNCEMENT
## RESEARCH ASSOCIATE
## IITA-TZ2023-R4D-001-NRS-DAR ES SALAAM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit **https://www.iita.org/** for more information about IITA.

IITA works with other CGIAR centres and national partners on the Seed Equal Initiative, which aims to strengthen seed delivery and improve farmer access to new improved varieties. Seed Equal is active across the global tropics, but has a diverse set of activities in Tanzania focusing on vegetatively-propagated crops. IITA also runs a project entitled BASICSII which is funded by the Bill and Melinda Gates Foundation and which has a vision of developing and commercializing the cassava seed supply chain from pre-basic seed of officially released varieties to community-level production by farmers.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the vacancy of the Research Associate - Seed Equal Initiative

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Dar es Salaam, Tanzania.

**Core Responsibilities:**
As a Research Associate, you will work as part of the Plant and Seed Health for Agriculture (PASHA) team of IITA-Tanzania, and will be responsible for supervising disease diagnostics activities in the molecular biology lab. This will involve ensuring the effective running of the lab, procuring lab consumables, conducting lab work including sample management, nucleic acid extracation, PCR-based diagnostics, LAMP assays and working with team members to expand the range of diagnostics being implemented. Additional tasks will include preparing and running virus diagostics training activities, working with team members on seed health studies, collecting field data from locations in Tanzania and elsewhere if required, and running screenhouse experiments. You will be expected to analyse, report and present results and contribute to the publication of scientific journal articles.

**Qualification, Experience and Key Skills**
- MSc in biological sciences with a minium of three years' experience in working in a molecular biology laboratory.
- Previous experience of working on laboratory diagnostics for viruses affecting root, tuber and banana crops will be a great advantage.
- Excellent communication and writing skills. Fluent English. For successful candidates who show strong research skills and high commitment levels, there will be an opportunity to study for a PhD.

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es Salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

17233602

## POSITION ANNOUNCEMENT
## RESEARCH TECHNICIAN
## IITA-TZ2023-R4D-002-NRS-DAR ES SALAAM

The International Institute of Tropical Agriculture (IITA) is a not-for-profit institution that generates agricultural innovations to meet Africa's most pressing challenges of hunger, malnutrition, poverty, and natural resource degradation. Working with various partners across sub-Saharan Africa, we improve livelihoods, enhance food and nutrition security, increase employment, and preserve natural resource integrity. IITA is a member of CGIAR, a global agriculture research partnership for a food secure future. Please visit **https://www.iita.org/** for more information about IITA.

IITA works with other CGIAR centres and national partners on the Seed Equal Initiative, which aims to strengthen seed delivery and improve farmer access to new improved varieties. Seed Equal is active across the global tropics, but has a diverse set of activities in Tanzania focusing on vegetatively-propagated crops. IITA also runs a project entitled BASICSII which is funded by the Bill and Melinda Gates Foundation and which has a vision of developing and commercializing the cassava seed supply chain from pre-basic seed of officially released varieties to community-level production by farmers.

IITA is looking for a suitably qualified person to fill the vacancy of the Research Technician – BASICSII Project

**Duty Station:** This is a Nationally Recruited Position, and the incumbent will be based in Dar es Salaam, Tanzania.

**Core Responsibilities:**
As a Research Technician, you will work as part of the Plant and Seed Health for Agriculture (PASHA) team of IITA-Tanzania. You will work with other members of the BASICSII project team to improve the efficiency and reduce the cost of pest and disease diagnostic tests being used to assure the health of cassava planting material. In doing so, you will work closely with project partner – the Tanzania Official Seed Certification Institute. Tasks will involve ordering lab reagents, running diagnostic tests (including standard PCR, real-time PCR and LAMP), conducting lab and screenhouse experiments to improve diagnostic tests, as well as analysing and reporting results. You will also conduct training activities to strengthen capacity in the application of improved pest/disease diagnostics.

**Qualification, Experience and Key Skills**
- BSc in biological sciences with some previous experience of working in a molecular biology laboratory.
- Previous experience of working on laboratory diagnostics for viruses affecting root, tuber and banana crops will be a great advantage.
- Excellent communication and writing skills. Strong English.

**General information:**
The initial contract for the position is for two years: renewable subject to performance and availability of funds. The duty station for the position will be IITA in Dar es Salaam. This is a nationally recruited position and IITA offers a competitive remuneration package.

**Applications:** Applications including curriculum vitae, copies of certificates, telephone number, email address, and names and addresses of two referees should be sent to the Country Representative, IITA-Tanzania, Plot No. 25, Mwenge – Coca-Cola Road, Mikocheni Industrial Area P.O. Box 34441, Dar es Salaam, Tanzania or by email to **IITA-Tanzania@cgiar.org**

Applicants are requested to please indicate the reference number for the position as indicated on the heading of the announcement in your application as well as on the subject of your email if sending by email. If sending by post or hand delivery, please indicate the reference number on your application as well as on the left-hand side of your envelope. **Please note that any applications without the reference indicated will be automatically disqualified.**

**Closing date:** Two weeks from the date of advertisement appearing in the newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.

17233602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wezi wa maji ni sawa na wahujumu

**BAADHI** ya wawekezaji wakubwa nchini wanaodaiwa kuiba maji na kusababisha ukosefu wa huduma hiyo kwa wananchi ni sawa na wahujumu uchumi.

Wawekezaji hao baadhi wanadaiwa kuchepusha maji na kupeleka kwenye mashamba yao kwa ajili ya umwagiliaji.

Tabia hiyo inapaswa kukomeshwa kwa kuwa huduma ya maji ni muhimu kwa uhai wa binadamu, wanyama na mimea.

Juzi Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alionesha kukerwa na tabia ya baadhi ya wawekezaji wakubwa kuiba maji na kusababisha ukosefu wa huduma hiyo kwa wananchi wenye uhitaji.

Wakati akiweka jiwe la msingi kwenye tangi la mradi wa maji ya Ziwa Victoria katika mji wa Tinde wilayani Shinyanga, maji ambayo yatakwenda pia katika mji wa Shelui wilayani Iramba mkoani Singida, alionesha

kukerwa na tabia ya baadhi ya watu kuiba maji wakiwamo wawekezaji wakubwa na kuviagiza vyombo vya dola na kamati za ulinzi na usalama kuwasaka wote na kuwachukulia hatua.

Ametoa amri kuwa wizi wa maji nchini uwe mwisho na kuwaagiza wawekezaji wanaotuhumiwa kuhusika kwenye hujuma hiyo, kama wana uhitaji mkubwa wa maji wachimbe visima badala ya kusababisha wananchi wengine kuteseka kwa kukosa huduma hiyo.

Alibainisha kuwapo kwa baadhi ya watu kuchepusha maji kwenye mito bila vibali na kuiagiza Wizara ya Maji kubomoa vizuizi walivyojenga.

Mamlaka za maji ambazo ndizo zenye dhamana ya kusimamia huduma hiyo pia zimeonywa kuacha kubambikia bili za maji wananchi na wanaosoma mita wasome kwa usahihi badala ya kukisia.

Pamoja na agizo hilo la Makamu wa Rais kwa wanaohusika na wizi na mamlaka za maji, lakini Watanzania wanajukumu kubwa la kuvitunza vyanzo vya maji likiwamo na Ziwa Victoria, pamoja na kupanda miti kwenye kingo ili kurejesha uoto wa asili.

Kuna baadhi wameamua kugeuza vyanzo hivyo kufanya shughuli za kilimo na wengine kudiriki hata kujenga na kuharibu mazingira yake.

Tukumbuke kuwa tunapofanya shughuli zozote za uharibifu katika vyanzo hivyo, tunajiweka wenyewe katika hatari ya kuvikausha vyanzo vya maji na kusababisha upungufu.

Dk. Mpango pia aliagiza wakaguzi pamoja na Baraza la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mabwawa yote ya taka sumu migodini ili kusitokee tatizo kama lilivyotokea katika bwawa la Mgodi wa Almasi Mwadui.


Pia Mthamini Mkuu wa Serikali ameagizwa kukamilisha uthamini haraka wa waathirika wa tope wa bwawa la Mgodi wa Almasi Mwadui ili walipwe fidia zao haraka na kuendelea na maisha yao.

Katika kusimamia suala hilo, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amehakikisha kuwa serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji kwa wananchi.

Katika Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, mji wa Tinde vitahudumiwa vijiji 22 na kunufaisha wananchi 60,000 pia maji hayo yanahudumia wananchi wa Shelui wilayani Iramba mkoani Singida na una gharama ya Sh. bilioni 24.4.

Ombi la wananchi na kuona maji hayo hayaishii kwenye tangi bali yasambazwe katika maeneo yao na kuanza kuyatumia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuache mtindo usiofaa kimaisha hata kukaribisha magonjwa haya

Na Sabato Kasika

**UGONJWA** wa kupooza unaotajwa na wataalamu wa afya kuwa unaathiri ubongo na ufanyaji kazi wake, ni hatari kwa maisha ya binadamu na mara nyingi hujitokeza ghafla.

Inaelezwa kuwa wakati mwingine, huwa kuna dalili ambazo mtu anaweza kupata kiashiria cha ugonjwa huo, kutegemea na sehemu ya ubongo iliyoathirika, ambayo ikiathirika zaidi inasababisha mtu kushindwa kuongea, kujitambua na kushindwa kurudi hali ya kawaida.

Mtu anapopata ugonjwa huo, seli za sehemu fulani ya ubongo hushindwa kufanya kazi kutokana na damu kushindwa kufika kwenye seli hizo za ubongo na huweza kuathiri sehemu yoyote ya ubongo na hivyo kuathiri ufanyaji wa shughuli za kila siku za mgonjwa.

Ugonjwa huo pia unaweza kusababisha mtu kupoteza maisha ghafla na kwamba ni muhimu kuwahi hospitali, kwa ajili ya matibabu, ambapo bila matibabu mazuri, kuna uwezekano mgonjwa kupata ulemavu wa kudumu.

Hata hivyo, suala la kulinda afya, ili kuepuka kukumbwa na magonjwa mbalimbali ukiwamo huo, limekuwa ni gumu kupewa uzito na baadhi ya watu, kitendo ambacho kinasababisha wakumbwe nao.

Mtindo wa maisha umekuwa ukitajwa kuwa chanzo cha yote hayo, ambapo sasa jamii inashauriwa kubadili mtindo huo, kwa kuwa sasa inaonekana kwamba bila jamii kubadilika inaweza kuendelea kuwa katika hatari.

Hii ni kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Dk. Respicious Boniphace, katika kambi ya mafunzo, kwa wataalamu wa upasuaji wa ubongo iliofanyika Dar es Salaam, wiki iliyopita.

Dk. Boniphace anasema, idadi ya wagonjwa wa kupooza wanapokelewa katika hiyo inazidi kuongezeka kila mwaka, huku chanzo kikiwa ni mtindo wa maisha uliopo sasa kwa watu wengi.

Ni kweli kama anavyosema daktari huyo kuwa watu wengi wamekuwa wakitumia magari, bodaboda na aina nyingine za usafiri kila sehemu wanapokwenda hata kama kuna umbali mfupi, tofauti na ilivyokuwa zamani.

Kwamba, zamani walimbeba kwa umbali fulani kwenda katika kituo cha daladala, lakini sasa mtu anapanda bodaboda kwenda kwenye kituo cha daladala hata kama hakuna umbali wa kiwango hicho.

Pia hata watoto wadogo nao hawapati muda wa kutembea, ambapo hata sehemu ndogo tu wanatumia usafiri, huku wengine wakiwa hawapati muda wa kucheza na kufanya miili kuwa imara.

Matumizi ya vyakula kama nyama choma, unywaji wa pombe nyingi, sigara na shisha bila ya kufanya mazoezi, navyo vinatajwa kusababisha mishipa ya damu kusinyaa na kuwa hatarini kupooza.

Inaelezwa kuwa, mazingira hayo huchangia magonjwa mengi kama presha au sukari na kwamba, hivi sasa vijana wa miaka 30 hadi 35 wanapata magonjwa ambayo zamani yaliwapata watu wazima wa kuanzia miaka 60 na kuendelea.

Kwa mtazamo wangu, takwimu hizi zinatosha kutushtua na kuchukua hatua, kwa kubadili mtindo wa maisha yetu ambao sasa unaonekana kuwa kikwazo kwa ustawi wa afya zetu.

Jambo la msingi ni kwa kila mmoja wetu kujitahidi kujikinga asipate ugonjwa huo kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya, kwani si rahisi kujua kwamba ukijitokeza utakuathiri kiasi gani.

Kimsingi, ni mtu kuachana na tabia hatarishi na kufanya mabadiliko fulani katika maisha yake ikiwa ni pamoja na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya ya kufanya mazoezi, kula na kunywa kiasi kinachokubalika.

Maelekezo mengine ya wataalamu wa afya ni kula mlo kamili, kudhibiti uzito, kupunguza chumvi katika vyakula, kwani wanajua athari zinazosababishwa na mtindo wa maisha yetu ya kila siku.

BancABC
part of
atlasmara

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa<br>31-Dec-22 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita<br>30-Sep-22 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,533 | 4,611 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,598 | 12,194 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,956 | 40,023 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,091 | 9,759 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 37 | 59 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 100,998 | 98,523 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 129,102 | 128,241 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 29,436 | 28,051 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,474 | 2,450 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **329,223** | **324,911** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 69,845 | 67,330 |
| 18 | Amana za Wateja | 138,213 | 139,084 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,181 | 2,185 |
| 28 | Madeni | 91,885 | 90,840 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **304,125** | **299,439** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **25,098** | **25,472** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 3,581 | 2,163 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (100,752) | (99,334) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,703) | (1,300) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,018 | 988 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **25,098** | **25,472** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 538 | 413 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 15,738 | 18,247 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,002 | 11,856 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 7.62% | 7.84% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.23% | 13.03% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.34% | 67.87% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39.21% | 39.47% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 46.63% | 46.40% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 0.80% | 0.00% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1.33% | 0.00% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa<br>31-Dec-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita<br>31-Dec-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa<br>31-Dec-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita)<br>31-Dec-21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,571 | 10,554 | 40,899 | 40,620 |
| 2 | Gharama za Riba | (5,115) | (5,427) | (19,878) | (20,403) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,457** | **5,127** | **21,020** | **20,217** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | (1,494) | - | (1,494) | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (1,340) | - | (1,340) | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,045** | **1,010** | **8,902** | **4,726** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 253 | 200 | 905 | 931 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 324 | 288 | 1,180 | 1,574 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 2,468 | 522 | 6,817 | 2,221 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(8,006)** | **(9,764)** | **(30,530)** | **(34,221)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,065) | (2,720) | (10,978) | (10,309) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,941) | (7,044) | (19,551) | (23,912) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(2,338)** | **(3,626)** | **(3,442)** | **(9,278)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (65) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2,403)** | **(3,783)** | **(3,703)** | **(9,557)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(2,403)** | **(3,783)** | **(3,703)** | **(9,557)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 177 | 167 | 177 | 167 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.98) | (1.54) | (0.38) | (1) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.94% | -1.12% | -1.13% | -2.71% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -38.02% | -11.27% | -14.65% | -33.66% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 94.16% | 162.27% | 102.03% | -136.11% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.06% | 0.72% | 2.94% | 1.75% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 DESEMBA 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa<br>31-Dec-22 | Robo Mwaka iliyopita<br>30-Sep-22 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (2,338) | (369) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 3,680 | 758 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (861) | 1,130 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,645 | (2,406) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,933) | 3,332 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,996 | (1,564) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (2,167) | (1,362) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (65) | (131) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(2,043)** | **(613)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (871) | (605) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(871)** | **(605)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 1,045 | 844 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **1,045** | **844** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,869) | (373) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 125,087 | 125,461 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **123,219** | **125,087** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 DESEMBA 2022

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (99,334) | 2,163 | - | 989 | 26,972 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,703) | - | - | - | (3,703) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 2,029 | 2,029 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,419) | 1,419 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (104,455) | 3,581 | - | 3,018 | 25,098 |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (89,329) | 1,715.64 | - | 989 | 36,329 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (9,357) | - | - | - | (9,357) |
| Hisa za upendeleo | - | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (447) | 447 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (99,334) | 2,163 | - | 989 | 26,972 |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 20-Jan-23 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 20-Jan-23 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 20-Jan-23 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 20-Jan-23 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 20-Jan-23 |

17236902

# China kuboresha matibabu ya moyo

**Na Halfani Chusi**

CHINA imekubali ombi la serikali ya kuongeza hospitali nyingine kubwa itakayoshughulikia magonjwa ya moyo.

Hatua hiyo imekuja siku chache baada ya Tanzania kuwasilisha ombi kwa serikali ya China kuomba kuongezewa jengo lingine kubwa kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wa moyo.

Katika kutekeleza ombi hilo, juzi, jijini Dar es Salaam, China na Tanzania zilitia saini mkataba wa kuanza kufanya upembuzi yakinifu kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila kwa ajili ya kuanza ujenzi huo mwakani.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema hatua hiyo itakwenda kuimarisha utoaji wa huduma hizo.

Alisema kwa sasa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKIC) inaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa moyo walioko nchini na nchi jirani licha ya kuwapo kwa kikwazo cha ufinyu wa eneo.

"JKCI inatoa huduma kwa wagonjwa wengi, waliolazwa hapa karibia wanafika 200, serikali ilipotembelea China mwaka 2018 iliwaomba wenzetu wa China kutusaidia kutanua jengo kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma hiyo kwa ufanisi zaidi.

"Baada ya ombi hilo, Serikali ya China ilituma wataalamu wakaja kuangalia uwezekano na tuliweka makubaliano kadhaa ya nini kinatakiwa kuboreshwa, leo tumesaini hizo 'minutes' za kikao hicho ambacho sasa kinaruhusu rasmi upembuzi yakinifu uanze kutekelezwa ili kuona namna ya kujenga hospitali.

"Kwa hiyo, hospitali hiyo itajengwa Mloganzila kwa makubaliano ya leo tunaanza rasmi kuangalia na namna ujenzi huo utakavyoendeshwa," alifafanua.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupunguza mrundikano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutokana na jengo hilo kuelemewa na wagonjwa.

Alisema jengo jipya ambalo litaanza kujengwa mwakani litachukua vitanda 300, akisisitiza litakuwa kubwa na lenye wataalamu watakaoweza kuhudumia wagonjwa kutoka ndani na nje ya nchi. "Mradi huu utaanza mwakani baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu. Kwa mujibu wa maelezo yao, utakamilika ndani ya miaka miwili, jengo litakuwa kubwa, ambalo litaweza kuhudumia na kutoa elimu juu ya magonjwa ya moyo kwa taasisi zaidi ya 50 kutoka nje ya nchi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kheri James, alisema wilaya yake itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati bila dosari yoyote.

# Waziri Mkenda ashtukia jambo digrii udokta wahitimu wa nje

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameipa rungu Bodi ya Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) kuchunguza ubora wa elimu na kutuma timu ya wataalamu kuhakiki tuzo zinazotolewa na baadhi ya vyuo vya nje.

Waziri Mkenda alitoa agizo hilo jana mjini hapa wakati akizindua bodi hiyo.

Alisema lengo ni kuwapa taarifa zilizosahihi Watanzania wanaotaka kupeleka watoto wao kusoma vyuo hivyo kwa kuwa ni jukumu la TCU kuwezesha na kudhibiti ili ubora wa elimu usitetereke. "Lengo si kuzuia wanafunzi kwenda kusoma kwenye vyuo hivyo bali kutoa taarifa kwa Watanzania kuhusu ubora wa tuzo zinazotolewa na vyuo hivyo hasa vinavyofundisha masuala ya udaktari, nilishaongea na balozi mbalimbali si vizuri kuzitaja timu iende na Katibu Mkuu kuangalia baadhi ya vyuo vikuu duniani ili kuhakiki," alisema.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya vyuo vinafundisha udaktari kwa njia ya mtandao na kueleza kuwa hajui kama vinamwandaa vizuri daktari kuja kufanya kazi nchini.

Aliagiza wahadhiri wanaoajiriwa ambao wana elimu ya Shahada ya Umahiri (Masters), kuwasilisha maandiko yao watu wasikilize.

"Kuna sehemu kubwa inatutaka kufanya ili kuongeza ubora, sehemu moja wapo vyuo vikuu vinafundisha walimu ambao wanakwenda kufundisha huku chini, halafu huku wanasema watu wanaohitimu vyuo vikuu hali si nzuri, kwa hiyo ni mzunguko kwa hiyo, vyuo vikuu ni muhimu kusimamia ubora wake kwa kuwa itakuwa ni chachu ya kusaidia kuongeza ubora huku chini," alisema.

"Kwa mfano tunapoajiri wahadhiri vyuo vikuu tusiangalie tu GPA tunaziamini, lakini kuna mambo mengi kuhusu GPA, tuwe na mahojiano, lakini na uwasilishaji lipo kwenye kanuni za TCU tusimamie.

"Kuna mtu alikuja kipindi kile nipo chuo kikuu akaja kuwasilisha andiko lake, lakini wakati tunampiga maswali tukajua huyu bogus (hana kitu), akaishia kusema ameandika haraka wakati sio kweli, alivyoondoka tukaangalia cheti amesema Norway na hana PhD kama alivyokuwa akisema."

Aliwakumbusha kuangalia suala la udanganyifu kwenye maandiko ya ngazi za elimu kwa wanaohitimu kutokana na baadhi yao kuanzisha ofisi za kuwaandikia watu.

"Napendekeza kwenu mfanye utaratibu wa kuchukua utafiti wao siku hizi kuna mfumo wa kutambua kama utafiti huo ni wa mtu, na ukipata hilo unatangaza kwa umma na aibu kwa chuo husika na msimamizi wa utafiti, unakuta mtu anasimamia watu 20 unawezeje?" Alihoji.

"Hizi ni salamu za vyuo vikuu tunataka hizi tuzo zihakikiwe, kwenye shahada ya Uzamivu ni vyema kuwe na utaratibu wa kutoa mawasilisho yao hadharani na umma usikilize badala ya watu wachache kujifungia kumpitisha kupewa tuzo ya PhD," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tume hiyo, Prof. Penina Mlama, alimhakikishia Waziri Mkenda kuwa watatekeleza maelekezo yote aliyowaagiza na kuifungua nchi kimataifa kwa kuwapeleka wanafunzi wengi kusoma vyuo vya nje ya nchi.

Prof. Mlama alisema bodi hiyo itahakikisha vyuo nchini vinasimama vyema kitaaluma kuhimili na kuyamudu mabadiliko ya kasi yanayotokea katika sekta zote za maendeleo binadamu, siasa, kiuchumi, kijamii na sayansi.


BancABC part of atlasmara

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |

| GENERAL CHARGES | | | |
|---|---|---|---|
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3%On small denominations above $500 | 3%On small denominations above $500 |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

| AGENCY BANKING FEE | | | |
|---|---|---|---|
| Deposit | Free | | |
| Bill payment | Free | | |
| **Withdrawal Fees** | | | |
| **Transaction tiers** | **BancABC Fees** | **Government Levy** | **Total Fees** |
| 0-999 | N/A | - | N/A |
| 1,000-1,999 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000-2,999 | 300 | 11 | 311 |
| 3,000-3,999 | 300 | 19 | 319 |
| 4,000-4,999 | 300 | 39 | 339 |
| 5,000-6,999 | 500 | 70 | 570 |
| 7,000-9,999 | 500 | 88 | 588 |
| 10,000-14,999 | 600 | 224 | 824 |
| 15,000-19,999 | 600 | 427 | 1,027 |
| 20,000-29,999 | 600 | 672 | 1,272 |
| 30,000-39,999 | 700 | 770 | 1,470 |
| 40,000-49,999 | 800 | 1,050 | 1,850 |
| 50,000-99,999 | 900 | 1,435 | 2,335 |
| 100,000-199,999 | 1,000 | 1,771 | 2,771 |
| 200,000-299,999 | 1,100 | 2,058 | 3,158 |
| 300,000-399,999 | 1,200 | 2,450 | 3,650 |
| 400,000-499,999 | 1,200 | 2,870 | 4,070 |
| 500,000-599,999 | 2,000 | 3,640 | 5,640 |
| 600,000-699,999 | 2,000 | 4,480 | 6,480 |
| 700,000-799,999 | 2,000 | 4,970 | 6,970 |
| 800,000-899,999 | 2,000 | 5,264 | 7,264 |
| 900,000-1,000,000 | 2,000 | 6,230 | 8,230 |
| 1,000,001-2,000,000 | 2,300 | 6,580 | 8,880 |
| 2,000,001-3,000,000 | 2,500 | 6,580 | 9,080 |
| 3,000,001 na zaidi | N/A | 7,000 | N/A |



## Manyara yajipanga kukusanya tani 2,500 za alizeti

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara kwa mwaka huu unatarajia kuvuna alizeti tani 2,500 kutoka kwa wakulima.

Taarifa ya Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti mkoani Manyara (MASUPA) iliyotolewa jana inaeleza kuwa alizeti hiyo itakusanywa kutoka kwenye vikundi vya wakulima wanaotambuliwa na chama hicho.

Jana, Katibu wa MASUPA, Julian Kambayta, alisema wamejiwekea lengo hilo la makusanyo kutoka kwa wasindikaji 239.

Alisema kila msindikaji amepewa jukumu la kwenda kukusanya alizeti kwa watu wake kwa bei ya mkataba ambayo hata hivyo hakuitaja.

Kambayta alisema hata kama bei ya zao hilo ikishuka, hawatanunua alizeti kwa wakulima kwa bei ya chini ya Sh. 800 kwa kilogramu moja.

"Wasindikaji tumewaunganisha na wazalishaji wa alizeti kwa makundi ili kuwapa wepesi wa kupata mali ghafi,"alisema Kambayta.

Akizungumzia uzalishaji huo, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalom Cheliga, alisema Vyama vya Ushirika Kilimo na Masoko (AMCOS), vinatakiwa kuzalisha kwa tija.

Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Rift Valley Cooperative Union (RIVACU), Vivian George, akizungumzia uzalishaji huo, alisema Mkoa wa Manyara una wakulima zaidi ya 3,000 ambao wanalima zao hilo.

Alisisitiza kuwa ili kufanikisha kilimo cha zao hilo, RICAVU imewaletea wakulima wa alizeti mbegu za kisasa kutoka kwa Wakala wa Mbegu nchini (ASA) ambazo ni nzuri na zina tija kubwa katika uzalishaji.

# Wanafunzi kutoka familia duni wapewa msaada wa mahitaji

**Na Thobias Mwanakatwe,**

NGORONGORO

WANAFUNZI 51 wanaotoka kwenye familia duni waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kutoka kata tatu za Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, wamepewa msaada wa vifaa na mahitaji mbalimbali ili kuwawezesha kwenda shule.

Msaada huo ulitolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo vikiwa na thamani ya Sh. milioni 12.

Misaada hiyo ni magodoro, masanduku, sare za shule, sabuni, taulo za kike, viatu, mikebe, mashuka, madaftari, kalamu, ndoo, limu pamoja na tishu.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro, Mohamed Bayo, alisema wanafunzi waliopata msaada huo wanatoka katika familia duni kutoka Kata ya Orgosorock, Enguserosambu na Oloirien.

Baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Bayo aliwataka wanafunzi hao wasiende kurubuniwa kwa mapenzi hali itakayowafanya washindwe kuendelea na masomo.

"Nyie mnatoka katika familia ambazo zina changamoto hivyo mnatakiwa mkasome kwa bidii ili baadaye mje msaidie wazazi wenu," alisema.

Alisema utaratibu wa kusaidia wanafunzi wanaotoka katika familia duni umeanza tangu mwaka 2021 baada ya kuanzishwa kwa mfuko maalum wa Diwani wa Kata ya Orgosorock.

Bayo ambaye ni Diwani wa Kata ya Orgosorock alisema mfuko huo tangu umeanzishwa umesaidia wanafunzi 104 waliochaguliwa kujiunga na shule za sekondari za serikali na zaidi ya Sh.milioni 24 zimetumika. Aliongeza kuwa mfuko huo ambao pia unaundwa kwa kushirikisha viongozi wa dini mbalimbali una lengo la kutaka kuufanya uwe mfuko wa wilaya ambao utawawezesha wanafunzi wote wanaotoka familia duni katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro waweze kunufaika.




Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Charles Makongoro Nyerere (kushoto), akifurahia jambo na Diwani wa Kata ya Mirerani, Salome Mnyawi (katikati), ambaye alijitolea shilingi milioni moja, kwa ajili ya kununua viti na meza vya Shule ya Sekondari Tanzanite juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro, Kiria Laizer. **PICHA: GIFT THADEY**

# Viuatilifu vyadaiwa kuhatarisha afya za wananchi Karatu

**Na Woinde Shizza,** KARATU

MATUMIZI ya viuatilifu vyenye kemikali za sumu za kuua wadudu waharibifu wa mazao zimelalamikiwa na wananchi kwamba zinahatarisha afya zao kwa kuwa zinaathiri mfumo wa hewa na upumuaji.

Wananchi hao ni kutoka Kata ya Endamag'a, Mang'ola na Baray zilizoko Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha.

Kwa mujibu wa Diwani wa Kata ya Baray, Elitumaini Rweyemamu tayari wamewasilisha malalamiko hayo kwa Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi, Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) jijini Arusha.

"Nimepokea malalamiko ya wananchi juu ya athari za dawa za kuua wadudu, ambazo zinatumika kwenye mashamba ya vitunguu. Ili kujadili suala hilo na kutafuta mwarobaini wake, nimelazimika kuagiza wenyeviti wa serikali za vijiji kuitisha haraka mikutano mikuu ya wananchi ili tuwaite pia watendaji wa serikali kusikiliza malalamiko yetu na kuja na majibu," alisema.

Alipoulizwa Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dady Kolimba, kuhusu malalamiko hayo, alisema hana taarifa hiyo lakini atafuatilia haraka kujua kinachoendelea katika kata hizo na kutoa kauli ya serikali.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wa kata hizo akiwamo Paselina John, alidai kuwa afya zao zipo hatarini kutokana na kuwapo mashamba makubwa ya vitunguu yanayolimwa katika makazi yao, ambapo wamiliki wake hutumia viuatilifu vya sumu kuua wadudu na hivyo kuathiri afya zao na baadhi yao kupata madhara ya kupumua.

Aidha, alisema dawa hizo pia zimekuwa zikiwaathiri wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Qand'end, wagonjwa wanaotibiwa katika Zahanati ya Lake Eyasi na nyumba za kulala wageni zilizozungukwa na mashamba hayo.

"Kwa kweli sisi wakazi wa Baray, tunapata tabu sana siku hizi kila eneo limegeuzwa shamba la vitunguu hadi kwenye makazi ya watu, wakianza kupuliza dawa za sumu, watoto wetu wanakohoa na kubanwa vifua hata shule hawaendi," alisema Paselina.


Kutokana na athari hizo, aliomba serikali kuwanusuru kwa kuwa malalamiko yao wameyafikisha ngazi mbalimbali lakini hawajapata ufumbuzi huku wakiendelea kudhulika.

Vilevile, Mathayo Babo, Mkazi wa Mbuyuni, alisema kwamba hivi sasa baadhi yao wanaishi maisha ya tabu kutokana na dawa zinazopuliziwa kuua wadudu kwenye vitunguu kufika hadi katika makazi yao na kuwaletea madhara.

"Hapo awali mashamba ya vitunguu yalijitenga umbali na makazi ya watu lakini watu wamevamia maeneo na kufanya uharibifu wa mazingira kwa kufyeka miti ya asili na kulima ovyo mashamba ya vitunguu," alisema.

Mkazi mwingine, Magreti Male, alisema amekuwa akiishi kwa shida yeye na watoto wake kupata mafua ya mara kwa mara na kubanwa vifua jambo ambalo alidai ni kutokana na athari ya dawa hizo zinazopuliziwa katika mashamba hayo na kuiomba serikali kuwanusuru na adha hiyo.

Muuguzi Mkuu katika Zahanati ya Lake Eyasi, Dk. Magreth Madila, alisema kuwa asilimia kubwa ya wagonjwa wanaokuja kutibiwa katika zahanati hiyo huwa wanakutwa na tatizo la mfumo wa upumuaji na hii ni kutokana na athari za viuatilifu vya dawa za kuua wadudu kwenye mashamba ya vitunguu.



# Wahamasishwa kulima vanilla kuondokana na utegemezi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wamehamasishwa kulima vanilla ili kujiongezea kipato cha kaya na kuondokana na utegemezi kwenye jamii.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Vanilla International, Simon Mkondya, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa elimu ya namna ya kulima zao hilo.

Alisema unapolima vanilla na kuihudumia ipasavyo mche mmoja unaweza kutoa kilo sita na kunahitaji unyevu kwa asilimia 85 kupitia shamba kitalu.

Mkondya alisema kabla ya kutoa elimu hiyo amefanya kwanza utafiti na kubaini kilimo hicho kinaweza kustawi vema wilayani humo na hekari moja ya zao hilo inaweza kutoa kilo 2,400 sawa na Sh. bilioni moja kwa kuuza kilo moja kwa Sh. milioni moja.

Alisema serikali imefuta kodi ya zao hilo ili kuhakikisha wananchi wanalima.

Mkondya alidai kuwa matunda mawili ya zao hilo nchini yanauzwa kwa Sh.18,000, Ujerumani yakiuzwa Sh.60,000 na kwamba mmea huo hauliwi na mnyama yoyote wala kushambuliwa na wadudu.

Aidha, alisema zao hilo linauzwa bei kubwa tofauti na mazao mengine ya biashara kwa sababu ikitengeneza pafyumu, inaharufu tofauti zaidi ya 500, kutengeneza dawa ghali, dawa ya usingizi, dawa za kutengeneza keki, soda, juice.

# Makamu wa Rais aonya wizi wa dawa hospitali za serikali

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameonya vitendo vya wizi wa dawa kwenye hospitali za serikali na kuviagiza vyombo vya dola kuwabaini watu wote ambao wanajihusisha na wizi huo na kuwachukulia hatua.

Alibainisha hayo juzi wakati akiweka jiwe la msingi katika Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga na kukemea tabia hiyo.

Alisema serikali imekuwa ikiwekeza fedha nyingi katika kuboresha huduma za afya hapa nchini, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na dawa ili wananchi wapate huduma bora za matibabu.

"Licha ya serikali kuboresha huduma za afya hapa nchini bado kuna matatizo ambayo yahahitaji kushughulikiwa, kama upungufu wa madaktari bingwa, watumishi, nyumba za madaktari na wizi wa dawa katika hospitali za serikali,"alisema Dk. Mpango.

Aliwaonya pia wauguzi na madaktari kuacha tabia ya kujihusisha na vitendo vya kuwaomba rushwa wagonjwa ndipo wawapatie matibabu, aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kulifuatilia suala hilo kwenye huduma zote za afya.

Aidha, aliagiza pia kwenye huduma zote za afya yatengwe madirisha ya wazee na yafanye kazi ikiwamo na upatikanaji wa dawa ili kuwapata kipaumbele wazee katika huduma za matibabu na kuimarisha afya zao.

Alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kuzingatia ushauri ambao umekuwa ukitolewa na wataalamu wa afya juu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko, ikiwamo Covid-19 na ebora, ili nchi ibaki kuwa salama dhidi ya magonjwa hayo.

Katika hatua nyingine alisema kutokana na Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga kukabiliwa na tatizo la barabara ya vumbi, Rais Samia ametoa Sh. bilioni saba ili ijengwe barabara ya lami kwenda kwenye hospitali hiyo.

Alisema licha ya kutolewa fedha hizo za ujenzi wa barabara kiwango cha lami, Rais Samia ametoa tena Sh. bilioni sita ili kujengwa majengo ya maabara na huduma za mama na mtoto.

Pia alikemea suala la mimba na ndoa za utotoni na kueleza limekuwa chanzo cha nchi kukosa wataalamu wake, wakiwamo madaktari bingwa na kuagiza tatizo hilo lishughulikiwe ili watoto wasome na kutimiza ndoto zao na kuja kulisaidia taifa lao.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema serikali itaendelea kutenga fedha za kuboresha huduma za afya hapa nchini na kueleza katika Mkoa wa Shinyanga kilishatolewa Sh. bilioni 19.5 ili kuboresha huduma hizo ikiwamo na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, waliishukuru serikali kwa kuendelea kuboresha huduma za afya ikiwamo na mkoa huo, ambao ulikuwa umesahaulika na walikuwa wakifuata huduma za madaktari bingwa katika Hospitali ya Bugando na Muhimbili na kusababisha gharama za matibabu kuwa kubwa.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango (kushoto), akimpongeza Naibu Meneja wa kampuni ya Uturuki inayojenga reli ya kisasa (SGR) ya Yapi Merkezi, Hana Alkan, baada ya kuzindua ujenzi wa reli hiyo Tabora-Isaka katika mji wa Isaka, mkoani Shinyanga juzi. Kulia ni Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehment Gulluoglu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aagiza viongozi wa shule kuhamasisha utunzaji mazingira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amezitaka shule zote za msingi na sekondari mkoani humo kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa kuweka kipaumbele katika upandaji miti kwenye maeneo ya wazi.

Amesema hatua hiyo ni sehemu ya kupambana na athari za mazingira zianazotokana na shughuli za kinadamu.

Alitoa kauli hiyo juzi wilayani Misungwi wakati akipokea vyumba 44 vya madarasa vilivyojengwa kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu.

Alisema kuwa upandaji miti utasaidia kurejesha hali nzuri ya mandhari na hewa safi ikiwa ni sambamba na kuwafundisha wanafunzi kupanda miti katika makazi yao. "Nimefurahishwa na hali ya upandaji miti katika shule hii walimu wamejitahidi kupanda miti katika maeneo yote ya wazi hali hii ipo pia katika Wilaya ya Magu natoa wito kwa viongozi wa shule zingine mkoani hapa kuiga mfano huu wa upandaji miti," alisema Malima.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alitembelea Daraja la Kigongo-Busisi na kuwahakikishia wananchi kuwa daraja hilo litakamilika kwa wakati.

"Niwaambie tu kuiba vifaa vya ujenzi wa miradi ya kimkakati ni kujiibia wenyewe na kuchelewesha maendeleo, hivyo hatutasita kupambana na mtu yeyote atakayefanya hivyo kwani huyo atakuwa mwizi," alisema Malima.



Ukurasa 12

PENYE NYUFA KISIASA, KIUCHUMI PANABOMOA UKUTA...
Rais Samia kafungulia mikutano ya kisiasa, zamu ya vyama sasa kulinda mitaji uchumi




Ukurasa 13

Hivi Watanzania tunajisikiaje kubagaza Kiswahili?


# BUFE

IJUMAA JANUARI 20, 2023

Nipashe





Ukurasa 14

Japan; kinara wa madeni duniani

KUKOMA KWA MGOGORO ARDHI MIAKA 15...

# Uamuzi wa Rais ulivyowaondolea mhemko, ukawasogezea tabasamu wakazi Mbarali

**NA Juma Mpagama, MBARALI**



Sehemu ya ardhi iliyochukuliwa uamuzi mzito na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kutangazwa rasmi wiki hii. **Picha kushoto**; Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiutangazia umma wiki hii kuhusu kilichoamuliwa. **PICHA ZOTE: OWM**

NI hatua ya kupumua, kunakosindikizwa na tabasamu kuanzia kwa wakazi hadi kwa watendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbarali, mkoani Mbeya, jalada na mgogoro wa ardhi kumalizwa.

Ni uamuzi mgumu uliochukuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kutatua mgogoro wa ardhi mkoani hapo, ulioudumu kwa miaka 15, ukiwahusisha wananchi wa Bonde la Usangu na kwenye Hifadhi ya Taifa Ruaha, hata ikawa inaleta kadhia kubwa ya kijamii.

Katika kuhakikisha mambo wilayani hapo yanakwenda vizuri kwa jamii hii ambao wanajulikana ni wazalishaji wakubwa wa mpunga, pia si haba katika ufugaji, Rais Samia akaamua kuridhia jumla ya hekta 74,000 zitumike kwa kilimo na ufugaji kwa wananchi.

Ni aina ya uamuzi ambao kiuchumi, inatafsiriwa inalenga kuondoa dosari na changamoto zinazochelewesha uchumi wa Taifa, kwa kuruhusu watu wapate vyanzo vya kujikimu kwa kupitia sekta mbalimbali zikiwamo kilimo na ufugaji.

Ni staili ambayo Rais Samia amekuwa akitumia, kila anapoona magumu ya kijamii na katika masuala ya kitaifa, amekuwa akiingilia moja kwa moja kwenye maisha ya umma na kurekebisha mahitaji yanayosukuma maendeleo yao.

Akizungumza kwenye mkutano wa wadau na wakulima wa mashamba ya mpunga, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anasema Rais Samia ameamua kuridhia suala hilo, akitaka wananchi waendeleze eneo hilo kwa ajili ya maendeleo yao.

Anasema serikali imefanya maboresho makubwa kwenye Tangazo la Serikali Namba 28, ambayo itawawezesha wananchi kufanya shughuli za kilimo na ufugaji endelevu kwenye eneo hilo.

Marekebisho ya tangazo hilo yatawezesha baadhi ya vitongoji vilivyokuwa vimetangazwa awali kuwa ndani ya hifadhi kuachwa nje ya mipaka, ikiwamo kutoa eneo la hekta 74,000 kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

"Rais Samia ameamua kuwa 'GN 28' itambue ufumbuzi baada ya vikao vingi na wadau kufanikisha, ikiwa hatua hii ni faraja kubwa kwa Watanzania wote.

"Nataka niwajulishe hapa Watanzania na wakazi wa Mbarali kuwa tumefikia hatua nzuri itakayowezesha kila anayejishughulisha na kilimo kuendelea na shughuli zake au hata wale wafugaji," anatamka Waziri Mkuu Majaliwa, aliyeambatana na timu ya mawaziri wahusika.

Anafafanua kuwa, serikali inanuia kuhakikisha Wilaya ya Mbarali inaendesha shughuli za kilimo kitaalamu na kwa tija, ndio maana wameamua kulitatua jambo hilo kwa kupewa baraka zote na maono ya Rais Samia.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Majaliwa, wameshaona maendeleo makubwa katika ujenzi wa viwanda kupitia watu mbalimbali, hivyo inakuwa vyema kama serikali haitaweki mipango mikakati ya kukuza uchumi wa nchi.

Kwa uamuzi huo, unaelezwa ni kupanua uzalishaji viwandani. Waziri Mkuu anaendelea mbele zaidi kwa kusema serikali imeamua kuitoa nje ya Hifadhi Ranchi ya Usangu kwa ajili ya shughuli za ufugaji wa kisasa.

"GN namba 28 iliingiza ranchi ndani ya hifadhi, lakini ili wafugaji wawe huru tumeiondoa na hivyo itakuwa nje, tumeacha na mito kadhaa ambayo itahifadhiwa kwa sheria za mazingira tulizojiwekea wenyewe kama Taifa.

"Tunawataka kuanzia leo wafugaji na wakulima wote mjiamini kwa sababu shughuli zenu zinakuza uchumi wa nchi moja kwa moja," anasema.

Anasema kuwa wadau hao wa maendeleo waondokane na uchungaji na kuwafanya Watanzania wafugaji kuacha kutembea umbali mrefu na ng'ombe kwani inaondoa thamani ya nyama, badala yake thamani ya nyama

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

PENYE NYUFA KISIASA, KIUCHUMI PANABOMOA UKUTA...

# Rais Samia kafungulia mikutano ya kisiasa, zamu ya vyama sasa kulinda mitaji uchumi

**Na Peter Orwa**

HADI sasa imekuwa jambo la wazi kwamba uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kufanya uamuzi wa kihistoria kunafungua milango ya mikusanyiko na mijadala ya kisiasa, imeleta neema na tabasamu la kisiasa.

Mara moja ikasikika kuwa viongozi kama Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti wa Chama cha CUF akiiitisha mkutano wa waandishi wa habari kuishukuru serikali akisifu kuwapo la ziada, hata wao wana - upinzani awali hawakuwahi kujumuika na kiongozi wa CHADEMA, Freeman Mbowe hadi pale kulipoitishwa mjumuiko na Rais Samia.

Pia kukasikika mikutano kama hiyo ya kiongozi wa ACT-Wazalendo, huku baada ya siku kadhaa, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA na mgombea urais katika kipindi kiliochopita, Tundu Lissu, anaangaza kurejea nchini wiki ijayo.

Itakumbukwa kuwa, hata Rais Samia alipokuwa katika ziara za kiuchumi nchini Ubelgiji, aliitikia ombi la faragha na Lissu, hata akayarejea 'mazungumzo yalikuwa mazuri.'

Hivyo, uamuzi wa Rais Saamia wa Januari 3, 2023 ambao kimsingi katika sura ya kawaida unaonekana unaanzia siasa, lakini mtazamo wa kina unagusa uchumi katika kile wanazuoni wanakiita 'multiplier effect', kwa maana ya jambo moja linafungua lingine.

Ni maeneo mengi Rais Samia, amekuwa akipigania ndani ya ulingo wake wa Tanzania vilevile ughaibuni akinuia kufungua milango mikuu, hasa katika masoko na uwekezaji wa mitaji katika maeneo muhimu kiuchumi.

Kufanikisha hilo, Rais Samia amefanya ziara nyingi za kimataifa ikiwamo kwa majirani Afrika Mashariki, katika Jamhuri ya China, pia Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na inaelezwa ishara ya rangi 'kijani' inaonekana.

Hapo akakamilisha kwa la ziada wiki mbili na nusu iliyopita pale alipoelekezea wigo wake baada ya kupumzika na ziara za kimataifa, akirejea kwenye kizimba cha demokrasia kwa mazungumzo ya kina na mamlaka za kisiasa kukaribisha 'ushoga' na 'uswahiba' kuanzia kwa wanasiasa hadi vyama vyao.

"Kwa hiyo, uwepo wangu leo mbele yenu ni kuja kutoa ruhusa, kuja kutangaza kwamba lile tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara limeondoshwa," akatamka Rais Samia.



Viongozi wa vyama vya siasa walipokutana na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

Tangu uamuzi wa kiserikali vyama vya kisiasa nchini 'ruksa' kujinadi kisasa, imeshusha pumzi kubwa ya malalamiko ya umma ya kisiasa, ikibeba hoja kuu ya marekebisho ya katiba, watu wakisubiri zaidi mikutano hiyo ambayo huenda wikiendi hii kukashuhudiwa kwa wingi.

### ANGALIZO LA RAIS

Tangazo la Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu la tarehe 3 mwezi huu, likanukuu maangalizo kadhaa ya rais:

- Vyama vya siasa kutumia mikutano ya hadhara kuikosoa na kuishauri serikali kistaarabu kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizoko.
- Serikali imedhamiria kukwamua mchakato wa kupata katiba mpya baada ya kukaa na kukubaliana na vyama vya siasa.
- Amebainisha kuwa mchakato huo wa katiba mpya utategemea hali ya nchi, uwezo wa kiuchumi, pamoja na mila na desturi.
- Serikali inajiandaa kurekebisha sheria anuai zikiwamo sheria za uchaguzi na sheria za vyama vya siasa, ili kujenga Taifa lenye umoja na ili liwe na umoja ni lazima kuwe na maridhiano.

Hayo ndiyo maeneo ambayo Rais Samia anapoeleza kwamba anakaribisha uwekezaji, hayo ndio mazingira rafiki ambayo majibu yake yanashuhudiwa kwa mifano ya viwanda na mradi mpya huko Mkuranga na Kibaha mkoani Pwani au katika Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam.

Ndani ya lugha Rais ni demokrasia na uchumi sasa zimepata ushindi kwa wakati mmoja. Ikirejewa hotuba yake, anakiri kuwapo haja ya ushirikiano wa wahusika hao nao katika upande wa pili wa shilingi, wanahusika moja kwa moja kutumia fursa hiyo kwa kumpa rais ushirikiano wa kulinda amani.

Katika kufanikisha, wahusika wamepewa vigezo kadhaa, viongozi wa kisiasa na vyama vyao kwamba; waendesha siasa za kistaarabu na kueleza ukweli wa mambo ulivyo ndani ya staha, kuwa mbali na fujo na vyombo vya ulinzi na usalama vipewe nafasi zao katika utekelezaji.

Wakati siasa ya namna hiyo itafanikishwa, ni wazi kwamba kiuchumi unafungua mazingira tajwa ya mwanzoni ya 'multiplier effect' na hata Rais Julius Nyerere, mwaka 1964 alinadi siasa ya uchumi ya Tanzania kwa kanuni kwamba "inawezekana, timiza wajibu wako."

### SURA YA MATARAJIO

Kuruhusiwa kwenye mikutano ya kisiasa ni jambo moja na nini kinatarajiwa kwenye mikutano ya kisiasa ni jambo lingine.

Majumuisho ya awali yanaonyesha ajenda na sera za kisiasa 'mtatufanyia nini' ndio imekuwa ikitawala zaidi kiatika mikutano ya kisiasa, huku ngome ya upinzani nayo ikitumia nafasi kubwa katika 'wametuangusha katika hili na lile.'

Dhana kuu katika yote inaangukia kuwa mada za kiuchumi ndizo zinabeba hisia za watu katika ajenda 'unatufanyia nini' ambayo ni shughuli za kimaendeo za moja kwa moja kuanzia uchumi, masoko hadi miradi inayowakimu kama vile shule, zahanati, maji, miudombimu ya barabara na umeme.

Vivyo hivyo, wawekezaji wa mifumo ya uzalishaji kama vile kilimo na viwanda, hali kadhalika masoko na biashara nao huangalia sana mambo makuu mawili ili waingize mitaji yao nchini; mosi wakiangaza katika kiwapo mahitaji muhimu kama vile umeme, barabara na sera rafiki, mambo ambayo Tanzania imepiga hatua.

Lakini kuna la pili ambalo hata Rais Samia anataka urafiki na ngome za kisiasa ni kwenye utulivu wa kisiasa na umma kwa jumla. Ni eneo ambalo likikosa utulivu, linarudisha nyuma juhudi hizo za kiuchumi.

Hapo ndipo suala hilo la utulivu wa nyendo wa kisiasa unahitaji nafasi hiyo kwa nadharia ileile iliyozalishwa na Hayati Mwalimu Nyerere kwa kauli ya mwaka 1964 "It can be done play your part' (inawezekana, timiza wajibu wako).

### UWEKEZAJI ULIKOFIKIA

Katika kuzingatia hali ya nchi, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), katika taarifa yake ya hali ya uwekezaji nchini katika mwaka wa fedha 2021/ 22 na mwelekeo wa mwaka 2023 bado inaonyesha ishara ya kuboreka, hivyo kuurejeshea umma nafasi ya kujenga utulivu kufikia hatau husika.

TIC inasema kufanikiwa kutokana na kuimarika shughuli za uratibu na utoaji huduma kwa wawekezaji kwenye sehemu moja (one stop facilitation centre), kasi ya usajili wa miradi kuwa juu na kuhamasisha uwekezaji.

Kati ya Juni 2021 na Julai 2022, jumla ya miradi 274 imesajiliwa ikilinganishwa na miradi 234 iliyosajiliwa katika kipindi hicho mwaka 2020/2021; ni sawa na ongezeko la asilimia 14.6.

"Miradi iliyosajiliwa katika kipindi hicho inatarajiwa kuzalisha ajira 43,925 ukilinganisha na ajira 36,470 zilizoripotiwa kipindi hicho mwaka 2020/2021," inafafanua taarifa hiyo.

Miradi hiyo inatajwa katika sekta za; viwanda, usafirishaji, kilimo, ujenzi/majengo ya biashara, miundombinu ya kiuchumi, taasisi za fedha, rasilimali watu, usafirishaji, utalii na huduma.

### MIRADI VIGOGO

Kuna jumla ya miradi sita TIC inataja kwamba, inatarajia kuwekezwa kwa kiasi cha dola za Marekani bilioni 1.10 na kuzalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 28,710. Pia zitaokoa fedha za kigeni zaidi ya dola za Marekani bilioni moja, ambazo zingetumika kuingiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Miradi hiyo ni kampuni; Itracom inayozalisha mbolea, mradi wa Knauf Gypsum, pia mwingine wa kampuni ya kuzalisha gesi.

Hali kadhalika, kuna kampuni mpya ya sukari ya Bagamoyo, ambayo pia itahusika na kilimo cha miwa; vilevile kuna mradi mipya kama hiyo ya sukari na miwa, ikiendeshwa na kampuni kongwe za Kagera Sugar na Mtibwa.

Katika kipindi kuanzia Juni 2021 mpaka Julai mwaka jana, kuna jitihada zimefanyika kuhamasisha uwekezaji kutoka nje, kukiandaliwa makongamano makubwa na idadi yake katika mabano, katika nchi za Misri (2), Kenya (1), Burundi (1), Ufaransa, Ubelgiji, Qatar, Uturuki, Afrika Kusini na Algeria.

## Uamuzi wa Rais ulivyowaondolea mhemko, ukawasogezea tabasamu wakazi Mbarali

**INATOKA UK.11**

itapanda endapo watafuga kisasa.

### MAWAZIRI WADAU

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, anasema kuwa maeneo ambayo yameondolewa katika hifadhi, watahakikisha mpango bora wa matumizi ya ardhi unawekwa, ili wananchi waweze kufanya kile ambacho kimepangwa kufanyika kwa wakati huo.

Anaeleza kwamba, kusudio kuu la serikali ni kuweka mkakati kabambe wa kuwapatia wananchi hao hati miliki za maeneo yao, ili wayatumie katika shughuli za maendeleo na mpango wa uandaaji utafanyika kwenye vijiji vinavyohusika.

"Hakuna njia nyingine ya mkato ya kwenda mbele kiuchumi kama mawazo hayo ya wakuu wetu wa nchi hayatawekwa katika misingi mizuri, hivyo sisi kama wizara tunaingia moja kwa moja kuliweka vizuri jambo hili," anasema.

Dk. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), anawataka wananchi waliaofikishiwa uamuzi huo, kuwa watiifu kwa kuheshimu sheria za mazingira yao.

Anawasihi jamii ya wafugaji kuwa, umefika wakati muafaka kwa wakulima hao na wafugaji kutii sheria, badala ya kufanya vitu tofauti, ingawa serikali yao ina malengo ya dhati juu yao, ndio maana imeona ilivalie njuga sakata la mgogoro huu wa ardhi.

Pia Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, anawataka watumiaji wa eneo lililotolewa kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kilimo waendelee kulilinda eneo lililobaki kwa maendeleo ya Taifa.

Anasema itakuwa vibaya kama eneo hilo lililobakia baada ya kumegwa, litaendelea kuvamiwa na wananchi kwa malengo tofauti.

"Nawaomba tusifuge wala kulima katika eneo lililobaki, kwa kuwa tunakitegemea kama chanzo kikuu cha utalii kwenye eneo hili," anasema.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, katika nasaha na ufafanuzi wake, anahimza kuwa Ranchi ya Usangu, ipo kwa ajili ya shughuli za ufugaji tu na kuwataka wananchi wasijaribu kuingiza shughuli nyingine tofauti.

"Tulioko kwenye ranchi tufuge, wengine mnabadilisha matumizi wengine hamfugi, lakini mnakodisha watu wanakuja kulima kwenye vitalu, wale mnaolima badala ya kufuga tutawanyang'anya vitalu," anasema.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Hivi Watanzania tunajisikiaje kubagaza Kiswahili?



**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
(kulangwasos@gmail.com)

KUNA nyakati, waandishi wa habari huonekana watu wa ajabu sana. Kwanini? Kwa sababu wanaweza kuwa wanaishi mahali fulani kuna habari, lakini wasiione.

Hubainika kuwa, hicho kilichoko ni habari baada ya mtu mwingine mgeni kufika mahali hapo na kubaini kuwa ipo habari na ndipo utaona waandishi hao nao kuichangamkia.

Hii ni kawaida kwa watu wote, kwamba unaweza kuwa na kitu kisicho cha kawaida nyumbani mwako, tena cha thamani kubwa, lakini usikione, mpaka aje mgeni akushtue.

Tanzania imekuwa hivyo siku zote, kwamba ina mambo mengi ya kifahari na ya kujivunia, lakini mara zote imekuwa ikijikuta ikijibeza yenyewe mpaka ishtuliwe.

Tumeshuhudia kwenye madini ya tanzanite, kwenye rasilimali zingine za wanyama na maliasili kedekede, zinazovutia mataifa mengine hata kuja kujionea kwa malipo.

Watanzania miaka nenda rudi tuliishi na vitu visivyo vya kawaida kama milima na hata maziwa, bila kujua kama vina thamani, mpaka walipokuja walioitwa wavumbuzi, kana kwamba hatukuwa tunaishi maeneo hayo.

Wakaja wengine, wakakuta tunatumia almasi kama kete kuchezea bao, wakatudanganya wakatubadilishia na shanga nasi tukakenua meno kwa furaha, huku wao wakinufaika nazo.

Tunajulikana duniani kama kitovu cha lugha ya Kiswahili, lakini bado hatuamini na tunaendelea kuamini Kiingereza! Dunia ina lugha zaidi ya 6,000, Kiswahili kikipewa nafasi ya saba, lakini bado hatuoni.

Dunia imetangaza Julai 7 ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani, lakini bado wazito, hatuelewi, tunashadidia Kiingereza na sasa tumeamsha mjadala wa Kiingereza kiendelee kutumika kufundishia na ikiwezekana hata chekechea!

Mtu na akili zake anasimama kadamnasi na kuhanikiza akilalamika kuwa inashangaza wanafunzi wa Kitanzania hawajui Kiingereza! Astaghafirulah, Kiingereza ni lugha mama ya Watanzania, kwamba asiyekijua hafai kuhesabiwa kuwa Mtanzania?

Yaani miaka yote hii ya uhuru, bado tunapanda basi la Kiingereza kweli? Inashangaza na kusikitisha, kuwa badala ya kusonga mbele tunarudi nyuma, hata hao wanaokiheshimisha Kiswahili, wanazidi kutushangaa.

Yaani mpaka leo hatujui kuwa kuna mataifa huko nje yanatamani kujua Kiswahili? Nchi jirani ya Kenya inajivunia Kiswahili kuliko hata sisi. Wamezagaa mataifani huko ughaibuni wakifundisha Kiswahili na kuaminisha kuwa chimbuko lake ni Kenya.

Leo, sisi badala ya kukitetea na kufanya haraka kutafsiri vitabu vya kiada na ziada vinavyotumika shuleni kufundishia, ndio kwanza tunakibagaza na kukiona kuwa ni cha kishenzi, kuwa aliyesoma ni anayejua Kiingereza.

Ugonjwa huu unatokana na ulevi tu, ambao unajibainisha pale baba mlevi anaporudi nyumbani kwake usiku na kugonga mlango huku akitukana: "You idiots open the door for me!" anafanya hivyo wakati mchana akiaga kwenda klabu cha pombe alifanya hivyo kwa Kiswahili!

Inashangaza kuwa si siku nyingi nyuma, tulishaamua (ingawa kinadharia) kuwa Kiswahili kitumike kufundishia shuleni, lakini sijui limetokea wimbi gani sasa tunajadili tena kitu kile kile, badala ya kusonga mbele, huku mahakamani baada ya tamko ilishaanza kutafsiri sheria!

Tatizo la Watanzania, ni wenye dhamana ambao wengi walisoma au kusomeshwa ughaibuni, ambako wanajua walilazimika kujifunza lugha za huko kabla ya kuanza mafunzo, ndio hao wanashadadia Kiingereza nchini.

Hawa ndio wenye watoto kwenye shule za Kiingereza wanazoziita za kimataifa na wengine wakisoma ughaibuni, lakini pamoja na kupewa nafasi serikalini, wanakuwa mstari wa mbele kukandamiza lugha mama yao!

Tulishakosea nyuma, kwa kuwa na utaratibu wa kufundisha masomo kwa Kiswahili kuanzia chekechea mpaka msingi na ghafla Kiingereza, sekondari mpaka vyuo. Hapo, lazima kigugumizi kiibuke katika Kiingereza.


Hivi tu ukiamua sasa, kwamba tunafundisha kwa Kiingereza tangu msingi, tunao hao walimu wakutufundishia watoto? Tufanye utafiti basi huko shuleni tuone kama tuna walimu wa Kiingereza hasa, kama siubabaishaji wa Yes! No!

Tukitaka kujijua tuko wapi, basi angalau siku moja ya Mkutano wa Bunge tuitenge mijadala iendeshwe kwa Kiingereza mchana kutwa, ndipo tutaona tunaning'inia wapi! Kiswahili ni lugha ya mama, hatujachelewa, tukae tutafsiri tufundishe kwa Kiswahili chekechea - chuo kikuu. Tujivunie kilicho chetu! Alamsiki!

UCHUMI

# Japan; kinara wa madeni duniani

## • Pata habari za nchi 10 tajiri duniani




Shughuli za biashara zikiendelea jijini Tokyo, Japan. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MNAMO Septemba mwaka jana, Japan ilikuwa na deni la umma lililofikia Dola za Marekani trilioni 9.2, ambayo ni asilimia 266 zaidi ya Pato la Taifa.

Kwa kulinganisha ile ya Marekani, ilifikia dola za Marekani trilioni 31 katika kipindi hicho, lakini kiuchumi ni sawa na asilimia 98 ya Pato la Taifa.

Sababu inatajwa, Japan imetumia miongo kadhaa kuongeza matumizi ya ndani, kuhudumia uchumi wake. Inatajwa matumizi ya raia wake yako katika mahitaji yasiyoendana na ya kiserikali na ukuaji uchumi kwa ujumla.

“Akiba binafsi ni kubwa na uwekezaji ni dhaifu, ikimaanisha mahitaji dhaifu,” anasema Takeshi Tashiro, Mchumi Mwandamizi katika Taasisi ya Peterson ya Uchumi wa Kimataifa, akifafanua kunashuhudiwa zaidi fedha katika akiba binafsi.

Sababu ya hali hiyo inatajwa ni kuwapo tatizo la idadi ya watu wake wengi ni wenye umri mkubwa, ambao huongeza gharama za usalama wa kijamii na huduma za afya serikalini na si wazalishaji zaidi.

> **“Uzee wa idadi ya watu unaochangia hali hii, unatarajiwa kuendelea kwa muda mrefu,” anaongeza mtaalamu huyo.**

“Uzee wa idadi ya watu unaochangia hali hii, unatarajiwa kuendelea kwa muda mrefu,” anaongeza mtaalamu huyo.

Hata hivyo inaelezwa kuwa, pamoja na uwapo wa deni hilo kubwa la umma, wawekezaji kimataifa wanaendelea kuiamini Japan, kwa kuikopesha fedha kupitia kununua madeni yake.

**CHANZO NINI?**

Deni la umma la Japan linatajwa lilianza kuongezeka mwanzoni mwa miaka ya 1990 na kuathiri fedha na mali isiyohamishika. Hadi kufika mwaka 1991, uwiano huo wa deni ulikuwa asilimia 39.

Kuanzia wakati huo, kasi ya ukuaji uchumi ulianza kushuka sana, hata ikapunguza mapato ya serikali, huku ikilazimisha kuongezeka matumizi yake.

Miaka 10 baadaye, zama za miaka ya 2000 deni la serikali lilivuka asilimia 100 na hadi kufikia mwaka 2010, lilikuwa limeongezeka mara mbili zaidi.

Inatajwa kukuzwa na matukio kama vile kushuka kwa uchumi wa dunia miaka ya 2008; Tetemeko la Ardhi la Fukushima na Tsunami iliyofuata 2011 na hivi karibuni zaidi janga la Covid 19, mahususi miaka ya 2020 na 2021.

**INAKABILI VIPI?**

Ili kupunguza athari za matukio haya na kudumisha bajeti ya kila mwaka katika maeneo kama vile elimu, afya au ulinzi, Japan kama karibu nchi zote duniani, huuza dhamana za serikali kwa watu na kampuni mbalimbali binafsi.

Kwa maneno mengine, inaweka deni lake katika masoko ya kimataifa kwa ahadi ya kumrudishia mwekezaji kwa ukamilifu wake pamoja na faida ndogo.

Wawekezaji hukopesha pesa zao kwa nchi hiyo, hasa wale wanaona hatimiliki hizo ni mahali salama pa kuweka pesa zao.

“Pamoja na mavuno yaliyopatikana, hati fungani kutoka nchi zilizoendelea zinaweza kutumika kwa urahisi kama dhamana ya mikopo,” anaongeza Mtaalamu Tashiro.

Deni la Japan limekuwa endelevu kwa muda na nchi haijaanguka kiuchumi, wataalamu wanaeleza sababu ni kuweka mavuno kwenye bondi za serikali, wawekezaji wanaolipa kidogo wakiwa na imani.

“Kuna wawekezaji ambao wanapendelea utulivu badala ya faida na ndiyo maana wanachagua Japan kuweka akiba yao ya ziada,” mwana - uchumi Shigeto Nagai anaelezea.

“Japan imeweka viwango vya riba vya chini sana. Ingawa kiwango cha deni ni kikubwa sana, serikali inalipa riba kidogo kwa wadai wake. Inaweza kuendeleza deni kubwa kwa muda usiojulikana,” anasema Ken Kuttner, Profesa wa uchumi katika Chuo cha Williams, kutoka Massachusetts, Marekani.

“Hakuna madeni mengi ya Kijapani yanayoshikiliwa na wageni. Ilikuwa karibu asilimia nane mara ya mwisho nilipoangalia. Mengi yanashikiliwa na taasisi za fedha za Japan na Benki ya Japan,” Profesa Kuttner, anasema.

**WAJUE MATAJIRI 10**

Kipimo kinachotumiwa kutafsiri ama utajiri au umaskini wa nchi ni Pato la Taifa, linalojumlisha uzalishaji bidhaa na huduma za nchi katika kipindi fulani na kuchukuliwa kama kiashirio cha utajiri wa eneo hilo.

Kipimo hicho huisaidia serikali kujua kiasi chake cha mapato, pia matumizi kwa huduma muhimu kama vile afya na elimu.

Kwa mujibu wa takwimu za Oktoba 2022 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa na Visual Capitalist, nchi hizo 10 tajiri duniani ni zifuatavyo, kiashiria ikiwa ni thamani ya Pato la Taifa katika thamani ya pesa, Dola za Marekani.:

1. Marekani; ina bilioni Dola 25.03.
2. China; Dola bilioni 18.321
3. Japan; Dola bilioni 4.301
4. Ujerumani; Dola bilioni 4.031.
5. India - dola za Marekani bilioni 3.469
6. Uingereza; Dola bilioni 3.199.
7. Ufaransa; Dola bilioni 2.778.
8. Canada; Dola bilioni 2.2
9. Russia; Dola bilioni 2.113
10. Italia; Dola bilioni 1.997

***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.**



## Bunge labaini upungufu wa usimamizi miradi ya mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imebaini kuwapo na upungufu wa usimamizi wa miradi inayotumia fedha za mikopo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, aliyasema hayo juzi baada ya kukutana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Alisema wameangalia utendaji kazi wa wizara hiyo kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 hasa kwenye miradi ambayo imetumia fedha za mikopo.

"Tulikuwa tunaangalia miradi ambayo imetumia fedha za mikopo ili kutekeleza miradi ile, kamati imekaa na kuangalia kwa undani, ripoti ya CAG imeonesha utendaji haukuwa mzuri," alisema. Alisema ilichukuliwa miradi sita kati ya 55 ambayo imeonesha kumekuwa na upungufu mkubwa katika Wizara ya Fedha na Mipango kusimamia miradi inayotumia fedha za mikopo ambayo inalipwa kwa kodi za wananchi.

"Kama wizara haitabadilika na kusimamia vizuri fedha hizi zinazokopwa ambazo mwananchi wa kawaida analipa kwa kulipa kodi, hakika nchi yetu itakuwa haifikii malengo yanayotarajiwa,"alisema.

Kaboyoka alisema: "Nchi inapochukua mkopo inatarajia mkopo ulete faida na matokeo chanya ili tunapolipa mkopo tulipe kwa kitu ambacho kimeleta maboresho katika uchumi wetu, lakini kama miradi inafanywa haifikii malengo, haikamiliki kwa wakati tunalipa riba kubwa kwa kuchelewesha kulipa makandarasi." Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema utekelezaji wa miradi hiyo haukusimamiwa vizuri na kusababisha tija na ufanisi kutokuwapo.

"Ucheleweshaji katika kufanya maamuzi unachelewesha utekelezaji wa miradi kwa mfano mradi wa usambazaji wa umeme unaitwa Backbone ambao unaunganisha Kenya na Zambia, ambapo hapa nchini kukiwa na upungufu tutapata umeme kutoka huko, utekelezaji wake umeonekana haukuwa mzuri," alisema.

Alitaja mradi mwingine ni usambazaji wa maji katika Jiji la Dar es salaam na kwamba wizara inatakiwa kujipanga kusimamia kikamilifu fedha zinazotokana na mikopo mbalimbali ili iwe na tija.

# Serikali yatakiwa kuongeza nguvu upatikanaji mafuta na mchele

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imesema serikali inapaswa kuongeza nguvu ya kuondoa upungufu wa mafuta ya kula na mchele kama ilivyofanya kwenye bidhaa ya sukari.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Kihenzile, aliyasema hayo jana baada ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuwakilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake pamoja na ya taasisi zake 16 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022.

Alisema kamati inapongeza wizara kwa jitihada mbalimbali ilizozifanya kutatua tatizo la upungufu wa sukari nchini ifikapo mwishoni mwa mwaka 2023 na kuitaka kuongeza nguvu kuondoa tatizo kama hilo kwenye mafuta ya kula na mchele. Pia alisema kamati hiyo imeiagiza wizara kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI) kwa wakati ili kurahisisha ufanyaji biashara na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini.

Nao baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walitoa maoni mbalimbali yaliyolenga kutatua upungufu wa mafuta ya kula na mchele, kutafuta masoko ya nje ya bidhaa mbalimbali ikiwamo bidhaa za mwani, uendelezaji wa maeneo maalumu ya kiuchumi, mifuko ya uanzishaji wa biashara ndogo, fursa za soko la AfCFTA na uanzishaji wa mfuko wa ubunifu.

Naye Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliihakikishia kamati hiyo kuwa wizara imepokea mapendekezo na maoni yote yaliyotolewa na itayafanyia kazi ili kuendelea kuweka mazingira bora na wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini na kukuza uchumi.

Awali akiwasilisha taarifa hiyo mbele ya kamati, Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ally Gugu, alisema katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022 wizara imeendelea kutekeleza jitihada mbalimbali katika kuendeleza sekta ya uwekezaji, viwanda na biashara.

Alisema jitihada hizo ni pamoja uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA ya utoaji huduma za pamoja, uendelezaji wananchi kiuchumi, utekelezaji wa miradi ya kimkakati, uratibu wa mahusiano ya kibiashara kikanda na kimataifa pamoja na upitiaji wa sera na sheria mbalimbali ikiwamo Sheria ya Uwekezaji 2022.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (kushoto), akizungumza na watumishi wakati akifungua mafunzo kwa idara ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za serikali jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ofisi ya Waziri Mkuu yatakiwa kuwezesha nguvu upatikanaji ujuzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, imeshauriwa kuendelea kuwezesha nguvu kazi kupata ujuzi ili kuondokana na tatizo la ajira nchini.

Ushauri huo ulitolewa jana na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kwenye kikao cha kupokea na kujadili taarifa ya ofisi hiyo kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotokana na taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati hiyo kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 na utekelezaji wa bajeti ya ofisi hiyo kwa kipindi cha nusu mwaka. Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Murtaza Giga, alisema kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na ofisi hiyo katika kutengeneza fursa za kuondokana na tatizo hilo na kutaka kuendelea kutilia mkazo eneo hilo. Akichangia katika kikao hicho, Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na ofisi hiyo katika kuwezesha nguvu kazi kupata ujuzi ni vyema kuangalia zaidi fursa za ajira za ujuzi mbalimbali zilizoko nje ya nchi ili kutatua changamoto ya ajira nchini.

Mbunge wa Viti Maalum, Zainab Katimba, alipongeza wizara hiyo kwa kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa vijana na kushauri kuendelea kupanua wigo zaidi.

Awali, akiwasilisha taarifa za ofisi hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema ofisi imetekeleza maazimio ya kamati ikiwamo kuimarisha mfumo wa uratibu ajira za Watanzania nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki katika michakato ya kuwaunganisha Watanzania na fursa hizo.

"Agizo lingine lilikuwa ni vijana wenye ulemavu wajumuishwe kwenye programu ya kukuza ujuzi pamoja na kwenye mkakati wa ajira katika miradi mbalimbali nchini, suala hili limetekelezwa na tumezindua mwongozo wa utekelezaji, ujumuishwaji na uimarishaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu wa mwaka 2022," alisema.

Waziri Ndalichako aliiahidi kamati hiyo kuwa ofisi yake itaendelea kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa kwa ubunifu.

Akijibu hoja mbalimbali za wajumbe wa kamati hiyo, Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema asilimia 50 ya vijana wa mafunzo tarajali wanaopelekwa kwenye sekta binafsi wamekuwa wakipata ajira kabla ya kumaliza muda wa mafunzo hayo. "Ofisi ya Waziri Mkuu tuna utaratibu mzuri wa kuwasaidia vijana ambao hawana uzoefu wanapata uzoefu kupitia programu ya kukuza ujuzi," alisema.

Kuhusu ulipaji wa mafao kwa wastaafu alisema kuna maboresho makubwa yamefanyika na sasa wastaafu wanalipwa mafao yao ndani ya siku 60.



## HABARI MBEYA



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akiteta jambo na mmoja wa wanawake waliofanyiwa upasuaji kwa lengo la kutibiwa ugonjwa wa fistula kwenye kambi iliyowekwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kitengo cha wazazi Meta jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Umaskini chanzo wanaougua fistula kukosa matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE 1,500 kati ya 3,000 wanaougua ugonjwa wa fistula kila mwaka nchini hukosa matibabu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali ngumu ya kiuchumi, umbali wa kwenda kupata matibabu na elimu ndogo kuhusu ugonjwa huo.

Mwakilishi wa Chama cha Madaktari wa Upasuaji wa Fistula Tanzania, Dk. Peter Majige, aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati wa uzinduzi wa kambi ya wiki mbili ya matibabu ya fistula inayofanyika katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kitengo cha wazazi Meta.

Kambi hiyo imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Hospitali hiyo, Chama cha Madaktari wa Upasuaji wa Fistula Tanzania na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji.

Alisema gharama za matibabu ya ugonjwa huo ni kubwa hali inayosababisha wagonjwa wengi kushindwa kumudu na hivyo kutojitokeza kutibiwa.

Alisema kutokana na hali hiyo chama hicho kimekuwa kikiomba ufadhili kutoka kwa wadau mbalimbali yakiwamo mashirika ya kimataifa ambayo yanasaidia mambo mbalimbali ya afya. Alisema kwa sasa wanafadhiliwa na Shirika la Fistula Foundation la nchini Marekani na kushirikiana na wadau mbalimbali kuandaa kambi katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wanawake wanaopata tatizo hilo.

"Tunaiomba serikali isamehe baadhi ya gharama za matibabu ya ugonjwa huu kwa sababu wengi wanashindwa kumudu matibabu, mwaka huu tumepata ufadhili wa kutibu kina mama 150 na tumeamua kuanzia Mbeya ambako tutatibu kina mama 60," alisema Dk. Majinge.

Alisema baada ya kukamilisha mkoani Mbeya wataendelea na matibabu katika mikoa ya Kigoma, Geita na Dodoma huku akieleza kuwa wafadhili hao hawagharamii chochote hali inayosababisha baadhi ya wagonjwa kushindwa kupata huduma.

Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Francis Rwegoshora, alisema hospitali hiyo inatoa huduma ya matibabu ya ugonjwa huo lakini wagonjwa wengi wanashindwa kufika kwa sababu ya kiuchumi.

Alisema kambi hiyo iliyopelekwa katika hospitali hiyo itasaidia kuyatambulisha matibabu hayo kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ya mikoa ya kanda ya nyanda za juu kusini ili waende wakatibiwe.

"Tunakushukuru sana Naibu Waziri kwa kuwashawishi madaktari hawa kuja kutoa huduma hii katika hospitali yetu, huduma hii ni muhimu sana kwa wanawake hawa maana ugonjwa huu unawafedhehesha sana wanawake," alisema Dk. Rwegoshora. Alisema tangu walipoanza kambi hiyo mpaka sasa wameshawafanyia upasuaji wanawake 15 kati ya 60 wanaotakiwa na hivyo akawataka wananchi kuchangamkia zaidi.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mahundi alisema ugonjwa huo umekuwa ukisababisha wanawake wengi kunyanyapaliwa kwenye jamii na wakati mwingine kukimbiwa na wenza wao jambo ambalo huwa linawaathiri zaidi. Alisema ugonjwa huo huwa unawasababishia maumivu makali wanawake huku ukiwaathiri kisaikolojia hasa pale wanaponyanyapaliwa na kukimbiwa na wenza.

# CHADEMA yalia na matatizo ya mfumo wa mbolea ya ruzuku

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeishauri serikali kushughulikia kero zinazoukabili mfumo wa uuzwaji wa mbolea ya ruzuku nchini ili kuwasaidia wakulima kupata bidhaa hiyo kirahisi na kuongeza uzalishaji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Bunge la Wananchi wa CHADEMA, Pascal Haonga, aliyasema hayo jana jijini Mbeya alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matatizo mbalimbali yanayoikabili sekta ya kilimo.

Alisema mfumo wa ruzuku ya mbolea unaotumika kwa sasa una matatizo mengi ambayo yanaweza yakalisababishia taifa njaa kutokana na kushindwa kuhudumia mazao yao.

Alisema mfumo wa ruzuku unaotumika kwa sasa umesababisha uhaba wa mbolea hasa kipindi hiki cha kukuzia mazao katika mikoa ya nyanda za juu kusini ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini.

Alisema uhaba huo unasababishwa na matatizo mbalimbali ikiwamo utoroshwaji wa mbolea kwenda nje ya nchi na baadhi ya watu ambao wanajiandikisha kama wakulima lakini wanakusudia kuziuza pembejeo hizo. Haonga alisema watu hao wamekuwa wakinunua mbolea hiyo kwa bei ya ruzuku ya serikali lakini wanasafirisha kinyemela na kwenda kuuza katika mataifa ya jirani.

"Hujuma hii imethibitishwa mara kadhaa na Waziri wa Kilimo na Waziri Mkuu walitembelea baadhi ya mikoa yetu ya nyanda za juu kusini lakini wamekuwa wakitoa kauli nyepesi kana kwamba ni upepo wa kawaida unapita," alisema Haonga.

Pia alisema serikali ilitenga bajeti ya ruzuku ya mbolea bila kufanya utafiti wa kutosha kuhusu mahitaji ya mbolea nchini jambo ambalo lilisababisha kutengwa fedha kidogo kwa ajili ya ruzuku hiyo.

Alisema kumekuwa na tatizo la wakulima kusafiri umbali mrefu kwenda kufuata huduma hiyo maeneo ya mjini ambako ndiko kwenye maduka yanayouza badala ya kusogezewa jirani na maeneo yao.

# Mabwawa sita kujengwa kuongeza tija uzalishaji wa mpunga

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetangaza kujenga mabwawa sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya kwa lengo la kuwezesha wananchi kuendesha kilimo cha umwagiliaji na kuongeza tija katika uzalishaji wa mpunga nchini.

Uamuzi huo ulitangazwa na Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mdolwa, wakati akiongozana na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, kwenda kukagua Bwawa la Rwanyo lililoko Kata ya Igurusi wilayani Mbarali ambalo ujenzi wake ulikwama kwa zaidi ya miaka 10.

Alisema lengo la serikali la kujenga mabwawa hayo ni kuifanya Wilaya ya Mbarali kuongeza tija kwenye kilimo kwa kuwafanya wananchi waache kulima kwa kutegemea mvua na badala yake waendeshe kilimo cha uhakika cha umwagiliaji.


"Serikali inakusudia kuifanya Wilaya ya Mbarali kuwa kitovu cha uzalishaji wa zao la mpunga nchini, azma hii itafikiwa kwa kuwawezesha wananchi kuongeza tija kwenye kilimo ikiwa ni pamoja na kuendesha kilimo cha umwagiliaji ambacho kitawafanya wakulima kulima zaidi ya msimu mmoja kwa mwaka," alisema Mdolwa.

Aidha, Mdolwa alisema kuwa lengo lingine la kujenga miundombinu ya umwagiliaji wilayani Mbarali ni kupunguza migogoro ya utumiaji maji baina ya wananchi na serikali kwa kuhakikisha maji yanatumika vizuri na ziada kurejeshwa katika Mto Ruaha kwa ajili ya matumizi mengine.

Alisema katika kufanikisha azma hiyo, serikali imeanza ujenzi wa skimu za kisasa katika maeneo mbalimbali wilayani Mbarali ambazo zitaepusha upotevu wa maji yanayoelekea mashambani kwa ajili ya kilimo ili baada ya matumizi yaweze kurejea mtoni. Mdolwa alisema kwa mwaka huu serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 61.6 kwa ajili ya ujenzi wa skimu sita za umwagiliaji wilayani Mbarali ambayo ujenzi wake unaendelea.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Anthony Mavunde, alisema serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji nchini ili kuongeza tija kwenye kilimo.






Vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu wakifanya mafunzo kwa vitendo katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji kisiwani Pemba, Zanzibar jana. Jumla ya vijana 600 wamenufaika na Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi (SDF) visiwani Unguja na Pemba kupitia mpango wa ufadhili kwa vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk. Mwinyi: BoT ni mdau muhimu wa maendeleo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ni mdau muhimu wa sekta ya maendeleo Zanzibar, pia ni mshauri mzuri kwa masuala ya uchumi wa nchi.

Aliyasema hayo juzi Ikulu, Zanzibar alipokutana na Gavana mpya wa benki hiyo, Emmanuel Tutuba.

Alisema Serikali ya Zanzibar inashirikiana vizuri na BoT na kwamba Zanzibar imepata mafanikio makubwa kupitia benki hiyo ambapo ushirikiano wa taasisi mbili hizo umejenga ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao ipasavyo.

Akizungumzia matatizo ya uchumi wa dunia, Dk. Mwinyi alimtaka Gavana Tutuba washirikiane kutafuta ufumbuzi mzuri wa kuzigeuza changamoto hizo kuwa fursa, ili zilete tija kwa taifa pamoja na kuziangalia kwa kuzidhibiti ili zisiathiri uchumi wa nchi.

Gavana Tutuba alisema BoT inafanya kazi kwa pande zote mbili za muungano katika kusimamia masuala ya kiuchumi na sera za fedha kwa Zanzibar na Bara.

Alisema serikali zote mbili zipo kwa ajili ya kulinda maslahi ya wananchi kwa kudhibiti mfumko wa bei duniani uliochangiwa na athari kubwa za kupanda kwa bei za mafuta ambayo inaathiri zaidi sekta ya usafirishaji kwa wananchi.

Katika hatua nyingine Dk. Mwinyi alikutana na uongozi na wafanyakazi wa Taasisi ya Benjamini Mkapa Foundation.

Katika mazungumzo hayo aliutaka uongozi wa taasisi hiyo, kuendelea kuboresha mifumo ya afya kwenye taasisi yao ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya taasisi hiyo, Balozi Tuvako Manongi alisema, bodi yao inashirikiana na taasisi mbalimbali, wadau wa maendeleo wakiwamo wafadhili kutoka sekta za umma na binafsi pamoja na wachangiaji binafsi katika kuhakikisha wanapata rasilimali fedha.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Ellen Senkoro, alisema taasisi hiyo imekusudia kuvitekeleza vipaumbele vyake vinne ikiwamo kuufanyia tathmini mpango mkakati uliopo wa taasisi hiyo ili kuongeza ubunifu na wigo wa kuanzisha miradi mipya baada ya mikongwe iliopo kukamilika kwa asilimia 50.

# Watatu mbaroni tuhuma kutapeli, kujifanya maofisa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar, imewakamata watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kuwatapeli wananchi kwa kujitambulisha kuwa ni maofisa wa mamlaka hiyo.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, Kamishna wa Mamlaka hiyo, Kanali Burhan Nassor Zuber, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Januari 16, mwaka huu, wakiwa katika harakati za kuwatapeli vijana wawili waliokuwa wamewashikilia na kuwabambikizia kesi ya kukutwa na dawa za kulevya kinyume na sheria.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Ramadhan Hassan Ali (36) mkazi wa Fuoni visiwani humo, Abubakari Khamis Ali (33) mkazi wa Tunguu na Rajabu Suleiman Ahmed (32) mkazi wa Jumbi.

Kamishna huyo alisema watuhumiwa hao waliwatapeli vijana wanne kwa viwango tofauti vya fedha ambapo Kijana Hafidh Iddi Juma alitapeliwa Sh. 600,000 na Juma Ali Said alitapeliwa Sh. 810,000.

Aliwataja wengine waliotapeliwa ni Ahmed Mustafa Simba Sh. 1,180,000, Ibrahim Abdullah Ameir Sh. 320,000 na Khalid Yussuf Mzee Sh. 200,000.

Alisema baada ya upelelezi kukamilika watuhumiwa hao watafikishwa kwenye vyombo vya sheria na adhabu stahiki kuchukuliwa dhidi yao.

# 'Uhuru wa habari ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya taifa'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, amesema uhuru wa habari ni nguzo muhimu katika maendeleo ya taifa.

Aliyasema hayo jana katika ofisi za TAMWA zilizoko Tunguu visiwani humo wakati wa mkutano wa uwasilisha wa Ripoti ya Sheria za Habari Zanzibar zilizofanyiwa mapitio, mkutano ambao uliandaliwa na TAMWA kwa kushirikiana na Shirika la Internews.

Alisema uhuru huo wa habari ni nguzo muhimu inayosaidia ukuzaji wa maendeleo kwenye nchi, hivyo inapotokea sheria ya tasnia hiyo kubana uhuru huo ni vyema kufanyiwa marekebisho.

Dk. Issa alisema kuna kila sababu ya kuona kwamba sheria, sera na matendo yaendane na mikataba ya kimataifa kuhusu uhuru wa habari ili kuleta maslahi kwa makundi yote.

Alisema azimio kubwa la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa (UN) ambalo lilitoka mwaka 1948 ambalo limeweka misingi mikubwa ikiwamo kila mmoja anahaki ya kutoa maoni na kujieleza bila ya kuingiliwa na kupokea taarifa na kueneza kupitia vyombo vya habari bila ya vikwazo.

Alisema Tanzania inapaswa kutekeleza hayo kwa sababu imeridhia mikataba hiyo ya kimataifa na kuna kila sababu ya sheria, sera na matendo kuendana na mikataba hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema kuna changamoto katika baadhi ya vipengele vya sheria ikiwamo Sheria Namba Nane, (27) (i) ya Wakala wa Habari Magazeti na Vitabu ambacho kinaeleza ofisa yoyote wa Jeshi la Polisi anaweza kuzuia au kukamata gazeti lolote lisichapishwe iwapo atashuku linakwenda kinyume na mikataba ya kimataifa kuhusu uhuru wa kujieleza.

Alisema kuwa hatua ya kufungia chombo ni jambo kubwa ambalo lisingepaswa kufanywa na waziri badala yake lilipaswa kufanywa na mamlaka nyingine ikiwamo Mahakama.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Shifaa Said kutoka Baraza la Habari Tanzania (MCT) Zanzibar, alisema licha ya juhudi kubwa kuchukuliwa na wadau wa habari kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya sheria mbalimbali lakini bado utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Aidha, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kufanya ushawishi wa mabadiliko ya sheria kwa kuandika mapungufu yaliyopo katika sheria hizo ili kufanyiwa marekebisho kwa haraka.

Akichangia ripoti hiyo mwandishi wa habari mwandamizi Zanzibar, Jabiri Idrissa alisema waandishi wa habari Zanzibar wanakabiliwa na mazingira magumu ya kufanya kazi.

Alitolea mfano wa Sheria ya Kinga na Madaraka ya Baraza la Wawakilishi namba 4 ya 2017, Spika anaweza kumuita raia yoyote wa Zanzibar kuhojiwa kwenye kamati za Baraza hilo iwapo ataona amefanya kosa ambalo limekinzana na Sheria za Baraza, huku sheria hiyo ikimzuia aliyeitwa kwenda na wakili wake wakati wa kuhojiwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**UYOLE HOSPITAL LIMITED**
**NAMBA YA USAJILI 28839**
**("Kampuni")**
**Uyole, Mbeya Tanzania**

## NOTISI YA KIKAO CHA MWISHO

Notisi hii inautaarifu umma kwamba kikao cha mwisho cha kufunga Kampuni tajwa hapo juu kitafanyika tarehe 30 Februari 2023 katika ofisi za Kampuni zilizopo Uyole, Mbeya Tanzania kuanzia saa 10:00 AM asubuhi. Agenda:

- Kupokea ripoti ya ufutaji kutoka kwa mfilisi.
- Kuweka bayana mahesabu ya Kampuni (kama yatakuwepo)
- Kujadili maulizo yote kutoka kwa wadeni wa Kampuni (kama watakuwepo)
- Mengineyo.

Kwa mamlaka ya mfilisi
VICTOR CHERUBIN MMOLE MKUMBE
Uyole, Mbeya 18th January, 2023.
Zunguko:
Kwa wanachama wote.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY RAJABU NDERA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T625 BRQ.** CHASSIS NAMBA **JTFA 426500012658.** ENGINE NAMBA **2KD1232653.** Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA.
**DAR/CHA/RB/18454/23.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANK JOHN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 647 CTC – TOYOTA RAV 4.** Chassis namba **ACA365001951.** Engine namba **1ACFE9568.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/498038/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAMWEL MAGESA SOSPETER** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 400 CRQ.** Chassis Namba **MD2B15BX1LWE90296.** Engine Namba **JVXWLE01594** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/300/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.132 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late GAITAN MGOGO LEMOJA**
**Of Dodoma Municipality/City at Mpunguzi**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MCHIWA GAITAN MGOGO**

**GENERAL CITATION**
**(Made under Rule 75 of Probate Rules)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **23 Day of January, 2023**

Date at Dodoma this **21 day of 12, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic company limited Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Gari jijini la Dar es salaam Mteja anashauriwa kulipa deni ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Novatus Beatus Tesha | TOYOTA VEROSSA T940DCR | 04.02.2023 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315 (Work ethic) au 0677014355 (Fanikiwa)**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......05/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: KONDO MFAUME WA MAFIGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA HAMISI KONDO**

**TANGAZO**
*(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 30 Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 01 mwaka 2023**

**HAKIMU MFAWIDHI**

HAKIMU

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MALEGESI M. MTAMWEGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S2354-0058** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **EAGLES SEKONDARI** November, **2015.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control number: **9910835598583.**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Waziri Mkuu New Zealand ajiuzulu

WAZIRI Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern, ametangaza kujiuzulu nafasi hiyo baada ya kueleza kuwa hana uwezo wa kutosha wa kuongoza nchi hiyo.

Ardern alijawa hisia alipokuwa akielezea jinsi miaka sita ya uongozi ukiwa na changamoto katika kazi hiyo ilivyomwathiri.

Atajiuzulu kama kiongozi wa Chama cha Labour kabla ya Februari 7, na kutoa nafasi ya upigaji wa kura katika siku zijazo ili kuamua mrithi wake.

New Zealand itafanya uchaguzi mkuu Oktoba 14, mwaka huu.

Ardern (42), alisema amechukua muda kufikiria mustakabali wake wakati wa mapumziko.


"Nilikuwa na matumaini kwamba ningepata kile nilichohitaji kuendelea katika kipindi hicho lakini, kwa bahati mbaya, sijapata na nitakuwa nafanya vibaya kwa New Zealand kuendelea," aliwaambia waandishi wa habari.

Kiongozi huyo alikuwa mkuu wa serikali mwanamke mwenye umri mdogo zaidi duniani alipochaguliwa kuwa waziri mkuu mwaka wa 2017, akiwa na umri wa miaka 37.

Alikuwa kiongozi wa pili kuchaguliwa duniani na kujifungua akiwa madarakani.

Aliongoza New Zealand kupitia janga la Covid-19 na mdororo wake uliofuata, mauaji ya msikiti wa Christchurch na mlipuko wa volkano wa White Island.

***BBC***




Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, akiwahutubia wajumbe waliohudhuria jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) kwa njia ya video mjini Davos juzi. **PICHA: AFP**

# Medvedev aonya NATO

**MOSCOW, Russia**

RAIS wa zamani wa Urusi ambaye ni mwandani wa Rais Vladimir Putin, ameionya Jumuiya ya Kujihami ya NATO kwamba kuna hatari ya kuanza kwa vita vya nyuklia iwapo Russia itashindwa katika vita nchini Ukraine. Medvedev ambaye anahudumu kama naibu mwenyekiti katika baraza la usalama lenye nguvu la Rais Putin, ameyasema haya kupitia ujumbe aliouandika katika mtandao wa Telegram.

Kiongozi huyo aliyehudumu kama rais wa Russia kati ya mwaka 2008 hadi 2012, alisema jumuiya ya NATO na viongozi wengine wa ulinzi ambao watakutana leo katika Kambi ya Kijeshi ya Ramstein nchini Ujerumani kujadili mikakati na uungwaji mkono wa juhudi za nchi za Magharibi kuishinda Russia nchini Ukraine.

Alisema wanastahili pia kufikiria kuhusiana na athari zitakazotokana na sera yao.

Russia na Marekani ndio wamiliki wakubwa wa zana za nyuklia, wakiwa na asilimia 90 ya zana za nyuklia duniani.

***DW***

## Wakenya watuhumiwa kupika gongo uarabuni

**NAIROBI, Kenya**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Kenya, Alfred Mutua, amesema kuna raia wa nchi hiyo ughaibuni wanaotengeneza pombe haramu katika nchi za Kiarabu ambako hairuhusiwi.

"Inasikitisha sana, kuna Wakenya ughaibuni wanatengeneza pombe za kienyeji 'chang'aa' na kuuza kwa Waafrika wengine kinyume na sheria za nchi za Kiislamu," alisema hayo katika mahojiano na kituo cha televisheni cha ndani, Citizen TV.

Alisema Wakenya wanaofanya shughuli haramu wanahujumu jitihada za serikali katika kushughulikia masuala ya ustawi wa raia wake nje ya nchi.

Alikuwa akijibu wasiwasi kuhusu baadhi ya Wakenya wanaokabiliwa na matatizo ikiwa ni pamoja na ripoti za unyanyasaji wa watu wanaofanya kazi Mashariki ya Kati.

Alisema serikali inafanya kila iwezalo kuboresha ustawi wa Wakenya huko.

Alisema aliona hali si mbaya na jinsi inavyosikika alipotembelea Saudi Arabia mara tu baada ya kuteuliwa kuwa waziri.

"Tatizo ni kwamba baadhi ya Wakenya hujihusisha na vitendo haramu na uhalifu wanapoenda huko," alisema.

***BBC:***

## Museveni akemea mapenzi ya jinsia moja

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ameonya dhidi ya kampeni zinazounga mkono haki za wapenzi wa jinsia moja nchini humo.

Sheria za nchi hiyo imeharamisha mapenzi ya jinsia moja.

Sheria ilisainiwa mwaka 2014 ambayo inaruhusu kifungo cha maisha kwa watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja na ndoa za watu wa jinsia moja.

Siku ya Jumatano kiongozi huyo alitaja haki za wapenzi wa jinsia moja kama ni upuuzi wakati wa hotuba aliyoitoa kwenye mahafali ya Chuo cha Kitaifa cha Ulinzi.

Aliongeza kuwa alifurahi kuhudhuria mkutano wa hivi karibuni nchini Marekani ambapo masuala ya haki za wapenzi wa jinsia moja hayakuzungumziwa.

***BBC***

# Iran yalaani Ulaya kutaka jeshi lake liorodheshwe kundi la kigaidi

**TEHREN, Iran**

IRAN imeukosoa mwito wa bunge la Ulaya wa kutaka Jeshi la Mapinduzi nchini humo kuorodheshwa kama kundi la kigaidi.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, ilisema Waziri Hossem Amir-Abdollahian katika mazungumzo kwa njia ya simu na mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, alikosoa vikali hatua hiyo ya bunge la Ulaya akisema haifai na si sahihi.

Juzi wabunge wa bunge la Ulaya walipiga kura ya kuifanyia mabadiliko ripoti ya kila mwaka ya sera za kigeni na kuutaka Umoja wa Ulaya kuliorodhesha jeshi hilo kama kundi la kigaidi.

Hakuna ulazima wa kutekelezwa kwa kura hiyo ila imefanyika wakati ambapo mawaziri wa mambo ya nje wa Umoja wa Ulaya wakiwa tayari kujadili kuibana zaidi Iran na vikwazo.

***DW***

HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS HAISHIKIKI, JKT IKING'ANG'ANIA KILELENI

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens iliyokuwa ugenini waliipa kichapo cha bila huruma Amani Queens cha mabao 7-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyangao mkoani, Lindi juzi.

Wakati Simba Queens ikifanya mauaji hayo, Maafande wa JKT Queens wakiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo waliendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo, walipoifunga The Tigers Queens kutoka Arusha mabao 2-0 huku Yanga Princess waliokuwa kwenye Uwanja wa Chuo cha Mkwawa, Iringa wakipata ushindi kiduchu wa bao 1-0 dhidi ya Ceasiaa Queens.

Mabao ya Simba Queens yaliwekwa wavuni na straika wa Oppa Clement aliyefunga mawili dakika ya 20 na 44, Mkenya Jentrix Shikangwa naye alipachika mawili dakika ya 50 na 60, pia mchezaji mwingine Mtanzania, Zainabu Mohamed 'Dudu' naye akfunga mabao mawili dakika ya 70 na 71. Mshambuliaji Asha Djafar ndiye aliyeanza kufungua ukurasa wa mabao kwa Simba Queens ambapo dakika ya sita alipachika bao la kwanza wakati goli pekee la Yanga Princess katika mechi hiyo ya juzi lilifungwa na straika raia wa Nigeria, Blessing Nkor.

Alliance Girls waliitwanga Mkwawa Queens mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza na Fountain Gate Princess wakaidungua Baobab Queens bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma jijini Dodoma.

Zilikuwa ni mechi za raundi ya sita ya Ligi Kuu ya Wanawake, JKT Queens ikiendelea kuongoza ikiwa na pointi 16, ikifuatiwa na Fountain Gate Princess yenye pointi 15, Simba Queens ikiwa kwenye nafasi ya tatu na pointi zake 13 kibindoni sawa na Yanga Princess lakini Wekundu wa Msimbazi wakiwa na idadi nzuri ya mabao ya kufunga.

Alliance Girls inakamata nafasi ya tano kwa pointi 10, Ceasiaa Queens iko katika nafasi ya sita pointi zake ni sita, Baobab Queens na Amani Queens zina pointi nne kila moja, huku The Tigers Queens na Mkwawa Queen zikiwa na pointi moja kila moja.




Washiriki wa kongamano la kujadili mapendekezo ya kumaliza changamoto ya ukatili wa kijinsia kwa wachezaji wa soka la wanawake hapa nchini baada ya kumaliza mkutano uliofanyika kwenye ukumbi wa TFF Ilala, Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

# NBC yakabidhi zawadi Bara

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambao mdhamini mkuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara, juzi ilikabidhi zawadi ya fedha na tuzo kwa Mchezaji Bora wa ligi hiyo wa Desemba, Clatous Chama pamoja na Kocha Bora, Juma Mgunda, wote kutoka Simba.

Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika muda mfupi kabla ya kuanza kwa mchezo wa Ligi Kuu kati ya Simba dhidi ya Mbeya City uliofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ambao ulimalizika kwa wenyeji kuibuka na ushindi wa mabao 3-2.

Katika tukio la makabidhiano ya zawadi hizo, ilishuhudiwa Mkurugenzi wa Udhibiti Majanga Benki ya NBC, Godliving Maro, aliyekabidhi mfano wa hundi ya fedha ya Sh. milioni moja kwa Chama pamoja na tuzo na kisimbuzi cha Azam huku pia zawadi kama hizo zikienda kwa Mgunda.

"Kimsingi sisi kama wadhamini tunaendelea kujivunia sana kuona ligi yenye ushindani na viwango bora vya kiuchezaji vinavyoendelea kuonekana kwenye ligi hii. Ndio maana utaona pamoja na ligi kuwa na wachezaji wengi wa kigeni bado wachezaji wazawa wanapambana na kufanya vizuri na wanachukua tuzo hizi. Huu ni uthibitisho vilabu vyote kwa sasa vinaweza kuhudumia vyema wachezaji wake kiasi cha kutoa ushindani unaotakiwa," alisema Maro.




Mkurugenzi wa Udhibiti Majanga wa Benki ya NBC, Godliving Maro (kulia), akikabidhi mfano wa hundi ya fedha ya thamani ya Sh. milioni moja kwa kiungo wa Simba, Clatous Chama, ambaye alitangazwa Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mwezi uliopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Global Peace, TFF, ZFF zapinga ukatili

**Na Saada Akida**

CHAMA cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), kimesema kitaendelea kushirikiana Taasisi ya Global Peace Foundation katika kuhakikisha changamoto ya Ukatili wa Kijinsia kwa Wachezaji wa Soka Wanawake unamalizika na kuendelea kuibua vipaji mbalimbali.

Katibu Mkuu wa TWFA, Somoe Ng'itu, tangu taasisi hiyo ilipoanza kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), katika kampeni hiyo, tatizo hilo limeanza kupungua kwa kiasi kikubwa kwa wachezaji kufahamu na kujitambua.

Somoe alisema watahakikisha wanaandaa mwongozo utakaosaidia wachezaji walioko na chipukizi kujitambua na kushiriki katika mchezo huo bila la kupata changamoto hiyo na baadaye kufanya vizuri.

"Hatua tulizofikia ni sehemu kubwa ya kazi tuliyofanya, tutaendelea kutatua au kusikiliza vilio au kuponesha donda linalowaumiza wachezaji wetu katika ukatili wa kijinsia ili kutimiza ndoto zao za kuiheshimisha Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa," Somoe alisema.

Naye mwakilishi wa TFF, Meneja Masoko, Aaron Nyanda, alisema shirikisho hilo linaungana na taasisi zote ambazo zinapingana na ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike.

"Tunahitaji kutokomeza au kumaliza hili kabisa kwa ajili ya ustawi wa soka la wanawake ili liendelee kukua na kuwa imara zaidi," alisema Nyanda.

Mkurugenzi wa Global Peace Foundation, Martha Nghambi, alisema taasisi yake itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wachezaji wa soka wanawake ili kuwasaidia kufikia malengo yao.

Alisema anaamini changamoto hii inaweza kumalizika endapo wachezaji watapata elimu ya kutosha katika kujitambua na watakaotenda makosa kuchukuliwa hatua.

Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Abdul-Latif Ally, alisema Global Peace Foundation inafanya jambo la msingi katika kuelimisha juu ya kujitambua kwa mtoto wa kike ili kuendeleza kipaji chake.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ALITAJWA LIVERPOOL

KLABU ya Paris St-Germain ilikuwa tayari kumruhusu mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe ajiunge na Liverpool msimu uliopita wa joto lakini alikataa mpango huo huku kukiwa na ripoti zinazomhusisha na Real Madrid. ***(Mail)***

### WEST YAMTAKA INGS

KLABU ya West Ham imetoa ofa kwa mshambuliaji wa Aston Villa, Danny Ings, mwenye umri wa 30, kwa nia ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji huku timu inayokabiliwa na hatari ya kushuka daraja ikihangaika kutafuta mabao. ***(Telegraph)***

### ARSENAL YAKATAA PRESHA

ARSENAL hawatoshinikizwa kununua wachezaji Januari baada ya kumkosa winga wa Ukraine, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 22, aliyehamia Chelsea na wako tayari kusubiri hadi msimu wa joto kabla ya kumnunua kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice (24). ***(Sun)***

### KOCHA ALIMBAKISHA MAGUIRE

WEST Ham ilijaribu kumsajili mlinzi wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 29, kwa mkopo lakini uhamisho wao ukakataliwa na Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, ambaye ana nia ya kumbakisha nahodha wa klabu yake Old Trafford kwa muda wote uliosalia.***(Mail)***

### MOYES ANUKIA EVERTON

KLABU ya Everton huenda ikashawishiwa kumchukua kocha wa zamani wa Manchester United, David Moyes mwenye umri wa miaka 59. ***(Sun)***

### GERNACHO, UNITED SAFI

KLABU ya Manchester United imewasilisha ofa ya mkataba ulioboreshwa kwa kinda wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 18. ***(Independent)***

### MAJA ANUKIA FULHAM

KLABU ya Fulham inahusishwa na mchakato wa kumnunua mshambuliaji, Josh Maja, mwenye umri wa miaka 24, kwa pauni milioni nne. Mshambuliaji huyo wa Nigeria, ambaye ni mzaliwa wa London, alikuwa kwa mkopo Craven Cottage mwaka 2021, amefunga mabao 11 katika mechi 19 alizoichezea Bordeaux kwenye Ligue 2 ya Ufaransa msimu huu. ***(Sun)***

### DEPAY MAMBO MAZURI

KLABU ya Atletico Madrid iko tayari kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, mwenye umri wa miaka 28 kwa ada ya pauni milioni 2.6. ***(Fabrizio Romano)***

### RAYA AGOMBEWA ENGLAND

KLABU za Chelsea na Manchester United ziko tayari kuchuana na Tottenham kwa ajili ya kumsajili kipa wa Brentford na Timu ya Taifa ya Hispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa joto. ***(Telegraph)***

### SPURS YAMTAKA PORRO

TOTTENHAM Hotspur imetoa ofa ya pauni milioni 30 pamoja na nyongeza kwa mlinzi wa Sporting Lisbon na Hispania, Pedro Porro, mwenye umri 23, lakini klabu hiyo ya Ureno inataka wafikie kipengele cha kuachiliwa kwa jumla cha pauni milioni 39.***(Record)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DEPAY AICHAGUA ATLETICO MADRID

●●●Mshambuliaji huyo anaamini akitua huko atapata nafasi ya kucheza ambayo...

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, yuko katika hatua za mwisho za kujiunga na Atletico Madrid.

Depay ambaye amekua akikosa nafasi ndani ya kikosi cha Barcelona yuko katika hatua za mwisho za kujiunga na Atletico Madrid.

... doka ili kwenda kupata nafasi ya kucheza ambayo ameikosa ndani ya Barcelona.

Mshambuliaji huyo ameripotiwa kujiunga na Atletico Madrid kwa uhamisho wa jumla tofauti na ambavyo iliripotiwa mwanzo kuwa angejiunga kwa mkopo, lakini mchezaji huyo atakwenda kwenye Atletico kwa uhamisho wa kudumu.

... taka mchezaji Hugo abaki, lakini ataelekea Atletico Madrid kwa uhamisho wa kudumu.

Depay alikuwa anasakwa na klabu mbalimbali za nchini England ikiwamo Manchester United.

Lakini mchezaji huyo ameamua kujiunga na Atletico Madrid kutokana na vipaumbele alivyoviizingatia mojawapo ni kupata nafasi ya kucheza.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,067,6

MECHI KALI
RB LEIPZIG
VERSUS
BAYERN MUNCHEN
1 | 3.62
X | 4.16
2 | 1.77

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALIYEMPIGA KIPA WA ARSENAL ASHTAKIWA




**LONDON, England**

SHABIKI mwenye umri wa miaka 35 amefunguliwa mashtaka ya shambulio baada ya kumpiga teke kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale, kufuatia kichapo cha mabao 2-0 cha Tottenham kwenye mchezo wa dabi ya kaskazini mwa London Jumapili.

Ramsdale, ambaye alisherehekea ushindi wa Arsenal mbele ya mashabiki wa Tottenham nyuma ya goli lake, alipigwa teke mgongoni na shabiki wa Spurs alipokuwa akienda kuchukua glovu zake baada ya mechi kumalizika.

Polisi wa Metropolitan walisema katika taarifa: "Mwanaume mwenye umri wa miaka 35 ameshtakiwa kwa kumpiga mchezaji wa Arsenal baada ya mechi kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur Jumapili."

Katika taarifa yao baada ya tukio hilo, Tottenham ilithibitisha shabiki huyo, baada ya kutambuliwa, atapigwa marufuku mara moja kuingia uwanjani.

"Tumeshtushwa na tabia ya shabiki aliyejaribu kumshambulia kipa wa Arsenal, Aaron Ramsdale mwishoni mwa mechi. Vurugu za aina yoyote hazina nafasi katika soka," ilisema taarifa ya Tottenham.

"Klabu imepitia picha zake za CCTV ili kumtambua shabiki huyo na itafanya kazi na Met Police, Arsenal na Aaron Ramsdale kuchukua hatua kali zaidi, ikiwa ni pamoja na kufungiwa mara moja kuingia kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur."

# Leao kubakia AC Milan

**MILAN, Italia**

WINGA wa kimataifa wa Ureno na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Italia, AC Milan, Rafael Leao, amekaribia kusaini mkataba mpya wa kuendelea kusalia ndani ya klabuni hapo.

Milan inapambana kuhakikisha Leao anasaini mkataba mpya kutokana na uwezo mkubwa ambao anaonyesha.

Milan imekua ikipambana kuhakikisha mchezaji huyo anasaini mkataba mpya kutokana na ushindani mkubwa ambao umekua ukiletwa na klabu mbalimbali za barani Ulaya ambao wamekua wakitaka huduma ya mchezaji huyo.

Leao amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu ndani ya AC Milan na kufanikiwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu Italia kwa msimu uliomalizika.

Milan kupitia Mkurugenzi, Paulo Maldini, wamekuwa wakizungumza juu ya nia yao ya kuhitaji Leao abakie klabuni hapo kusaini mkataba mpya.



## HABARI MICHEZO

615,605/-

# MUUZA DUKA SINGIDA ALAMBA MILIONI 7.8/- ZA SUPA JACKPOT

**Na Mwandishi Wetu**

MJASIRIAMALI Farhani Abdalla (pichani), kutoka Minga, Singida, wikiendi iliyoisha alijishindia kitita cha Sh. milioni 7. 8 cha Supa Jackpot bonus ya Sportpesa, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 14 kati ya michezo 17 iliyowekwa kwenye Jackpot ya wikiendi iliyoisha.

Akizungumza katika ofisi za SportPesa Oysterbay, Dar es Salaam, baada ya makabidhiano ya mfano wa hundi, Farhani alisema alianza kucheza na Sportpesa mwaka 2022 baada ya kuona na kuvutiwa na matangazo ya washindi wa Jackpot bonus.

Farhani alisema yeye anatabia ya kuangalia mechi za Jackpot zilizotoka mara nyingi siku za Jumatatu na baada ya hapo huchukua kama siku mbili au tatu kufanya utafiti na maamuzi ya kuweka mkeka.

“Mimi huwa na kawaida ya kila Jumatatu asubuhi kupitia magazeti ya mwananchi au mwanaspoti na kuangalia kuna timu gani ambazo zipo kwenye Jackpot katika wiki hiyo.”




Baada ya kujiridhisha kwa namna ambayo nimechambua timu za Jackpot, huwa naweka takriban mikeka 10 au 20 na baada ya hapo hutulia kusubiria majibu pale mechi zinapoanza kuchezwa.

“Kwa mkeka huu ulioshinda Jackpot bonus niliziona timu siku ya Jumatano na baada ya kuchambua kwa siku mbili niliuweka Ijumaa na baadaye nilitulia kusubiria matokeo. Kwa kweli hamna kipindi kigumu kama wakati wa kusubiria matokeo. Presha huwa inakuwa juu sana.”

Alisema fedha aliyopata ataongeza mtaji kwenye biashara yake na pia nyingine atapeleka katika kilimo kwa sasa yupo katika hatua ya kupalilia.

Farhani amewashauri Watanzania kucheza na SportPesa kwani ni kampuni ya uhakika na huduma zao ni za uhakika na malipo ni kwa wakati.

“Nachukua fursa hii mimi kama mshindi kuwapa ushuhuda wangu kwamba Sportpesa haina mbambamba.

Naye Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Farhani na kumtaka aendelee kucheza bila kuchoka kwani kuna siku kitita chote cha bilioni moja na ushee kitakuwa chake.

“Kwanza nakupongeza kwa ushindi huu wa Jackpot bonus. Pili naamini Jackpot bonus hii itakuwa chachu ya wewe kuendelea kuisaka Jackpot yenyewe ili na wewe katika siku za usoni uwe mshindi mkubwa.”

Supa Jackpot yetu wiki hii imesimamia 1,067,615,605.

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 21/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Nottingham Forest | 2.60 | 3.20 | 2.65 |
| 02. 21/01/23 | 18:00 | Southampton FC vs Aston Villa | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 21/01/23 | 18:00 | Birmingham City vs Preston North End | 2.38 | 3.10 | 3.10 |
| 04. 21/01/23 | 18:00 | Blackpool vs Huddersfield Town | 2.27 | 3.15 | 3.20 |
| 05. 21/01/23 | 18:00 | Cardiff City vs Millwall FC | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 06. 21/01/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.70 |
| 07. 21/01/23 | 18:00 | Wigan Athletic vs Luton Town | 2.75 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 21/01/23 | 18:15 | Espanyol Barcelona vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.15 | 2.55 |
| 09. 21/01/23 | 22:00 | SC Cambuur vs Sparta Rotterdam | 2.95 | 3.35 | 2.31 |
| 10. 21/01/23 | 23:00 | RKC Waalwijk vs Go Ahead Eagles | 2.36 | 3.45 | 2.80 |
| 11. 22/01/23 | 13:30 | Gaziantep FK vs Sivasspor | 2.50 | 3.30 | 2.75 |
| 12. 22/01/23 | 15:00 | Sunderland AFC vs Middlesbrough FC | 2.80 | 3.25 | 2.45 |
| 13. 22/01/23 | 16:30 | Feyenoord Rotterdam vs Ajax Amsterdam | 2.85 | 3.55 | 2.28 |
| 14. 22/01/23 | 17:00 | Leeds United vs Brentford FC | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 15. 22/01/23 | 17:00 | AC Monza vs Sassuolo Calcio | 2.26 | 3.30 | 3.10 |
| 16. 22/01/23 | 18:30 | Maritimo Madeira vs Estoril Praia | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 22/01/23 | 19:30 | Borussia Monchengladbac vs Bayer Leverkusen | 2.70 | 3.80 | 2.31 |

# MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## IJUMAA - 20/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 3482 | Bali Utd Pusam vs PSM Makassar | 2.14 | 3.21 | 3.11 |
| 12:00 | 5822 | Sheikh Russel KC vs Dhaka Abahani | 3.16 | 3.32 | 2.07 |
| 13:30 | 1954 | Gorilla FC vs Police FC Rwanda | 2.95 | 2.69 | 2.57 |
| 14:00 | 1808 | Gokulam Kerala FC vs Real Kashmir | 2.19 | 2.85 | 3.42 |
| 14:30 | 5716 | Persepam MU vs Persib Bandung | 2.46 | 3.11 | 2.69 |
| 15:30 | 2584 | Al Khaleej Club vs Al Raed Club | 2.41 | 3.41 | 2.77 |
| 16:00 | 1722 | Maccabi Jaffa vs Hapoel Acre | 2.52 | 3.26 | 2.73 |
| 16:00 | 1792 | El Fahem vs Bnei Yehuda | 2.20 | 3.10 | 3.42 |
| 16:00 | 5588 | Geita Gold FC vs Polisi Tanzania | 1.47 | 3.73 | 6.62 |
| 16:00 | 5951 | SC Kfar Qasem vs Hapoel Kfar Saba | 2.53 | 2.99 | 2.94 |
| 16:10 | 1867 | City Football Club vs Emirates Club | 8.70 | 5.18 | 1.26 |
| 16:30 | 5019 | Gasogi United vs Kiyovu Sports | 3.58 | 2.85 | 2.13 |
| 17:00 | 1794 | Shabab Alsamu vs Islami Qalqilya | 1.47 | 4.10 | 5.61 |
| 17:00 | 3580 | Shabab AL Amari vs Shabab AL Khaleel | 9.10 | 5.07 | 1.26 |
| 17:00 | 3749 | East Bengal vs Hyderabad FC | 4.85 | 3.72 | 1.60 |
| 17:30 | 1187 | Universitatea Cluj vs Voluntari | 2.22 | 2.95 | 3.43 |
| 18:00 | 4834 | Al Masry Club vs Ghazl EL Mahallah | 1.58 | 3.63 | 5.97 |
| 18:30 | 1235 | Boca Juniors vs Racing Club | 2.50 | 2.99 | 2.73 |
| 19:00 | 2473 | Istra vs Slaven Belupo | 2.33 | 3.06 | 2.91 |
| 19:00 | 5327 | Angola vs Mauritania | 2.37 | 2.85 | 3.35 |
| 20:00 | 1787 | Sakaryaspor vs Altinordu | 1.75 | 3.58 | 3.99 |
| 20:00 | 2105 | Olympiakos Nicosia vs AEK Larnaca | 6.83 | 4.16 | 1.46 |
| 20:00 | 4933 | Adana Demirspor vs Giresunspor | 1.66 | 3.94 | 4.58 |
| 20:00 | 5258 | Ceramica Cleopatra vs Smouha Club | 2.10 | 2.88 | 3.98 |
| 20:30 | 3094 | Sekhukhune United vs Moroka Swallows FC | 2.13 | 2.95 | 3.69 |
| 20:30 | 3939 | Cape Town City vs TS Galaxy FC | 2.02 | 2.95 | 4.06 |
| 20:30 | 4125 | Sochaux vs Caen | 2.37 | 3.01 | 3.06 |
| 20:30 | 5410 | Al Taawon vs Al Shabab Riyadh | 3.19 | 3.56 | 2.10 |
| 21:00 | 5676 | Rapid Bucuresti vs Sepsi Osk | 2.63 | 3.05 | 2.68 |
| 21:30 | 1323 | Panetolikos vs PAS Giannina | 2.27 | 2.91 | 3.44 |
| 21:30 | 1335 | Nancy vs Orleans | 2.08 | 3.11 | 3.53 |
| 21:30 | 3493 | Chateauroux vs Avranches | 1.53 | 3.99 | 5.47 |
| 22:00 | 1048 | Willem II Tilburg vs FC Eindhoven | 1.86 | 3.51 | 3.83 |
| 22:00 | 2332 | Den Bosch vs Jong PSV | 2.73 | 3.47 | 2.32 |
| 22:00 | 2662 | SBV Excelsior vs FC Volendam | 2.26 | 3.53 | 2.83 |
| 22:00 | 3046 | Congo vs Niger | 2.69 | 2.79 | 2.94 |
| 22:00 | 4708 | Almere City vs De Graafschap | 2.37 | 3.46 | 2.67 |
| 22:00 | 4995 | FC Arouca vs Portimonense | 2.25 | 3.22 | 3.12 |
| 22:00 | 5176 | PEC Zwolle vs VVV Venlo | 1.44 | 4.52 | 5.89 |
| 22:00 | 5345 | FC Oss vs NAC Breda | 2.84 | 3.32 | 2.32 |
| 22:00 | 5584 | Maastricht vs Heracles Almelo | 4.42 | 4.15 | 1.62 |
| 22:30 | 1690 | RB Leipzig vs Bayern Munchen | 3.62 | 4.16 | 1.77 |
| 22:45 | 3520 | Newry City AFC vs Glentoran Belfast | 7.69 | 4.47 | 1.34 |
| 22:45 | 4551 | Portadown FC vs Carrick Rangers | 3.07 | 3.43 | 2.07 |
| 22:45 | 5524 | Eupen vs Racing Genk | 5.77 | 4.58 | 1.46 |
| 22:45 | 5761 | Sheffield Utd vs Hull City | 1.60 | 3.71 | 5.35 |
| 23:00 | 1565 | Mallorca vs Celta Vigo | 2.80 | 2.85 | 2.75 |
| 23:00 | 5078 | Las Palmas UD vs Mirandes | 1.63 | 3.48 | 5.57 |
| 23:00 | 5821 | Burnley vs West Bromwich | 2.08 | 3.17 | 3.52 |
| 23:10 | 4108 | Marseille vs Rennes | 2.23 | 3.38 | 3.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# ROBERTINO AWATULIZA

INATOKA UK. 24

na kocha (Robertinho) aliona hilo na kufanya mabadiliko kwa ajili ya kufikia malengo yetu ya kutafuta pointi tatu jambo ambalo tumefanikiwa,” alisema Chama.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Abdallah Mubiru, alisema wachezaji wake wamepambana lakini bahati haikuwa upande wao kwa kuruhusu kupoteza mchezo huo jambo ambalo halikuwa katika malengo yao.

Mubiru alisema malengo makubwa katika mchezo huo yalikuwa kutafufa pointi tatu au kuondoka na alama moja licha ya kuamini wao ndio walitawala mpira kwa asilimia kubwa dhidi ya Simba.

“Niwapongeze wachezaji wangu kwa kuonyesha mchezo mzuri dhidi ya Simba iliyopata ushindi baada ya kutumia mapungufu yetu, tunaenda kujiandaa na mchezo ujao,” alisema Mubiru.

Simba itasafiri kuelekea Dodoma kuwafuata wenyeji Dodoma Jiji FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa na baada ya hapo itarejea Dar es Salaam kuwasubiri Coastal Union kwenye mchezo wa hatua ya 32 Bora ya mashindano ya Kombe la FA.

Wekundu wa Msimbazi ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati watani zao Yanga wao watachuana katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu zote zimetinga hatua ya makundi.

# YANGA YAITANGAZIA

INATOKA UK. 24

msimu huu.

“Tunaiheshimu timu hiyo, Ruvu Shooting ni miongoni mwa timu zenye ushindani kwenye Ligi Kuu, tutaingia uwanjani tukicheza kwa tahadhari kubwa,” Kaze alisema.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema wamefanya usajili mzuri katika dirisha dogo ambao umeimarisha kikosi chao na hawana hofu ya kukutana na mabingwa hao watetezi.

“Tumejipanga na tumejiandaa kuwakabili kwa kuwaonyesha ubora wetu, kikosi chetu sasa kimeimarika na kina mabadiliko, wasitarajie mteremko,” Bwire alisema.

# Michezo

Ijumaa Januari 20, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Depay aichagua Atletico Madrid



Wachezaji wa Simba wakishangilia bao la tatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilipata ushindi wa mabao 3-2. **PICHA: SIMBA SC**

# ROBERTINO AWATULIZA MASHABIKI MSIMBAZI

## ●●●Awaambia kwa sasa muhimu ni kupata pointi tatu ili kujiimarisha katika mbio...

**Na Saada Akida**

HUKU kukiwa na maoni tofauti baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa Simba , Roberto Oliveira 'Robertinho ' amesema kwa sasa anahitaji kupata ushindi bila kujali wachezaji wake wanachezaje kutokana na ushindani uliopo katika mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo.

Simba iliibuka na ushindi wa mabao 3-2 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ikiwa ni mechi ya kwanza kwa Robertinho, Saido Ntibazonkiza akifunga magoli mawili na lingine likipachikwa wavuni na Pape Osman Sakho.

Akizungumza na gazeti hili, Robertinho, alisema jambo lake la kwanza alikuwa anahitaji kuvuna pointi tatu muhimu, jambo ambalo alifanikiwa na limemfanya afurahie ushindi huo wa mechi yake ya kwanza.

Robertinho alisema amefurahishwa na namna wachezaji walivyocheza kwa ushirikiano licha ya kukaa nao kwa muda mfupi, wameonyesha kile alichowaelekeza katika siku chache alizokaa nao.

"Nilihitaji ushindi bila kujali tumechezaje, tupo katika mbio za ubingwa, tunapaswa kushinda kila mchezo hasa tunapokuwa nyumbani, ndio kwanza nina siku nane tangu nilipoanza kazi, Simba ni timu kubwa na malengo yake ni makubwa kama nilivyo mimi.

Jambo jingine lililonifurahisha ni jinsi tulivyocheza, wachezaji walicheza kitimu ingawa kulikuwa na makosa kadhaa ambayo tunapaswa kuyaondoa, nimeanza kupata mwanga wa kikosi ambacho kinapaswa kiwe, ninaimani mechi zijazo watacheza vizuri zaidi ya mechi ya leo (juzi)," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema kuhusu mabadiliko aliyoyafanya ni baada ya mchezaji wake kupata majeraha na kuogopa kuendelea kumtumia kwa sababu ya kuhofia kumuumiza na kupata jeraha kubwa zaidi na kufanya kukaa nje kwa muda mrefu.

Kuhusu kiungo, Clatous Chama, alisema aliondolewa baada ya kupata maumivu ya mguu na kuhitaji kufanyiwa mabadiliko kwa sababu hakuwa na uwezo wa kuendelea kuipambania timu.

"Nashukuru Mungu nilifanikiwa kutoa pasi na kupata bao la kwanza, nilisikia maumivu mguuni na sikuweza kuendelea kucheza na kuonyesha kiwango kizuri

INAENDELEA UK. 23

## Yanga yaitangazia hali ya hatari Ruvu

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

TATIZO la kukosa umakini limeendelea kumuumiza kichwa Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, ambaye alisema safu yake ya ushambuliaji inashindwa kutumia vyema nafasi wanazotengeneza na kushindwa kupata idadi kubwa ya mabao katika michezo wanayocheza.

Nabi alitoa kauli hiyo kufuatia timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu katika mchezo uliopita na kuongeza anahitaji nyota wake wabadilike na kupata ushindi mnono watakapoikabili Ruvu Shooting kesho usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema tayari ameanza kuyafanyia kazi mapungufu aliyoyaona ili kuhakikisha wanarejea wakiwa imara katika mechi inayofuata huku akiamini idadi kubwa ya mabao inaweza kuwasaidia katika kutimiza malengo yao mwishoni mwa msimu.

Alisema maandalizi ambayo wanayafanya yatawapeleka mahali wanapopahitaji na wameingia kambini mapema kwa ajili ya kuhakikisha wanapata mabao mengi katika kila mchezo.

"Tumekuwa tukishinda mabao machache kitu ambacho sijaridhika nacho, tumeanza mazoezi ya kufunga kwa washambuliaji, hivyo naamini kuanzia kwa Ruvu Shooting tutakuwa na mabao ya kutosha.

Kila mechi kwetu ni ngumu, tunawaambia wachezaji kazi yetu ni kusaka ushindi, wanaelewa na tutakwenda kupata matokeo chanya katika kila mchezo ili kufikia malengo yetu ya kutetea ubingwa," alisema Nabi.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedric Kaze, alisema wachezaji wao wanaendelea vyema na mazoezi kuelekea kwenye mchezo huo ambao pia utakuwa na ushindani.

Kaze alisema anafurahi kuona kila mchezaji anayepata nafasi anaonyesha kiwango kizuri, hivyo anaamini wataendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Baada ya kupata pointi tatu katika mchezo wetu uliopita dhidi ya Ihefu, sasa hivi tunaelekeza nguvu zetu kwa kuwaangalia Ruvu Shooting, tunaifahamu ni timu nzuri na hutoa ushindani kila tunapokutana nao, hautakuwa mchezo rahisi," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema mchezo huo utakuwa na upinzani mkubwa kwa sababu kila timu imejipanga vizuri

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >